**JECHA** afariki dunia, Rais Samia, ZEC na wanasiasa wamlilia



UKURASA 3

**MIAMALA** ya simu yaongezeka, tozo zashuka kwa bil. 4/-

UKURASA 18




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatano Julai 19, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII


ISSN 0856 • Na. 0581376

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Ulanguzi mafuta watikisa



**EWURA** yachukua hatua walioho-dhi nishati... *Endelea ukurasa wa 2*

## Samia aikaribisha Hungary fursa za uwekezaji nchini

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Rais wa Hungary, Katalin Novák, baada ya kuwasili Ikulu, Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 15

### MZEE AFARIKI DUNIA KWA KUNG'ATWA NA NYUKI

MKAZI wa Kikuyu jijini Dodoma, Abinel Chikataa (71), amefariki dunia kwa kung'atwa na nyuki kwenye sherehe za kuwatoa watoto suna.



UKURASA WA 17

### WANNE WAKAMATWA KUTAPELI WANANCHI

WATU wanne wamekamatwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja kwa tuhuma za utapeli katika maeneo yanayotoa huduma za kifedha Zanzibar.

UKURASA WA 7

### MBARONI TUHUMA KUOA MWANAFUNZI

JESHI la Polisi mkoani Songwe linamshikilia Lukia Magwaza (21), mkazi wa Kijiji cha Shasya, Kata ya Halunga wilayani Mbozi kwa tuhuma za kumwoa mwanafunzi (jina limehifadhiwa) aliyetakiwa kujiunga na kidato cha tano....

## 500 wapatiwa matibabu moyo JKCI kila siku

UKURASA 4

**MICHEZO** **STRAIKA MPYA WA YANGA AFUNGUKA** UK. 24 **KATUNI** UK. 6




Mkurugenzi wa Mawasiliano na Masoko wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Dk. Mohamed Maguo (kushoto), akitoa ufafanuzi kwa wananchi waliotembelea banda la chuo kwenye maonyesho ya 18 ya elimu ya juu, sayansi na teknolojia katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Tanzania yaikaribisha Hungary fursa uwekezaji

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewakaribisha wawekezaji kutoka nchi ya Hungary kuja kuwekeza Tanzania na kuongeza wigo wa kiuchuni hususan katika nishati mbadala, utalii, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), madini na sekta ya kilimo.

Rais Samia aliyasema hayo jana, Ikulu, jijini Dar es Salaam akiwa na Rais wa Hungary Katalin Novák, wakati wakizungumza na vyombo vya habari.

Rais Samia alisema miongoni mwa majadiliano kati yake na Rais Katalin ni pamoja na kukuza fursa za kiuchumi na namna ya kuongeza wigo wa uhusiano kwa nchi hizo mbili.

"Tumekubaliana kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya nchi zetu ili kuruhusu majadiliano, kukuza biashara na uwekezaji, kwa mwaka 2022 biashara ilikuwa ya Dola za Kimarekani bilioni 4.2 ingawa kuna uwezekano wa kuongeza wigo huu.

"Ninatarajia na kuwahakikishia kwamba serikali yangu itaweka mazingira wezeshi kwa wa-Hungary wanaotarajia kuwekeza Tanzania," alisema Rais Samia.

Kuhusu uhusiano katika sekta ya elimu kwa nchi hizo mbili, Rais Samia alisema Hungary imekuwa mshirika mzuri hasa kwenye elimu ya juu kwa kuwa wamejadiliana namna ya kunufaika na programu tofauti za kielimu na kwamba miongoni mwa yaliyowekwa saini kiutekelezaji ni sekta hiyo.

"Tunanufaika kwa pamoja kwa wa-Hungary kuja nchini kusoma kwenye vyuo vyetu na kwa mwaka huu tumeanza na watano huku Hungary ikiwachukua 30, tutaendelea kuongeza idadi kwa siku zijazo," alieleza Rais Samia.

Kwenye utalii Rais Samia alisema kwamba Tanzania ilipokea watalii kutoka Hungary 7,188 na kwamba idadi hiyo inaweza kuongezeka baada ya kuwasili kwa rais wa nchi hiyo nchini.

"Ziara hii ya kazi itaongeza uhusiano wetu kati ya Tanzania na Hungary, katika nchi ambayo itakuachia kumbukumbu hasa utakapotembelea kwenye vivutio vyetu vya utalii Serengeti, Ngorongoro mkoani Arusha na Moshi (Kilimanjaro)," alisema Rais Samia.

Aidha, Rais Katalin alisema ni hatua kubwa kwake kufika nchini na ziara hiyo ina maana kubwa kwa kuwa waliokutana ni viongozi na marais wanawake.

Alisema kukutana kwao kama marais, kunahamasisha wasichana walioko kwenye nchi zao kutokata tamaa na kufikia hatua ya kuwa mama ama kufanikiwa kielimu.

"Wote tunaamini kwamba kuwa mama ni jambo muhimu maishani. Haijalishi kwa kiwango gani au tofauti zetu kitaaluma, lakini hatupaswi kukata tamaa katika jinsi zetu. Tunahamasisha wanawake wote dunia kutokata tamaa, kuelekea mafaniko," alisema.

"Hungary tupo takribani watu milioni 10. Tuna taifa lenye heshima. Lakini tumekuja Tanzania kujifunza pia heshima yenu kama taifa, pamoja na kukuza ushirikiano.

"Tulizungumza na Rais (Samia) kuhusu hali tunayopitia kama nchi kwa kuwa Hungary tunapakana na Ukraine na vita inayoendelea imetuathiri pia, tumekwishapokea wakimbizi zaidi ya milioni mbili kutoka Ukraine na tuna changamoto za kiuchumi. Tulipoteza raia katika vita," alisema.

Kwa mujibu wa Rais Katalin, kuna fursa ya elimu kupitia scholarship (ruzuku ya masomo) zipatazo 12,000 kwenda kusoma Hungary kutoka nchi tofauti duniani ikiwamo Tanzania na kufadhiliwa masomo.

# Ulanguzi mafuta watikisa

**Na Waandishi Wetu**

ULANGUZI wa mafuta ya petroli na dizeli umedaiwa kukithiri katika mikoa inayopakana na nchi jirani baada ya wafanyabiashara kuyaficha ili kutengeneza uhaba waweze kupandisha bei.

Jana Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imewaonya wanaohodhi na kulangua mafuta hayo.

Nipashe imefuatilia uhaba wa nishati hiyo mkoani Songwe na kubaini kuwa kwa sasa mafuta yanauzwa kati ya Sh. 4,000 hadi 5,000 ikiwa ni mara mbili ya bei elekezi.

Aidha, Nipashe imebaini uhaba huo umeanza kujitokeza siku tano zilizopita baada ya vituo mbalimbali katika miji ya Vwawa na Mlowo kutokuwa na bidhaa hiyo, huku katika mji wa mpakani wa Tunduma vituo vichache vikionekana kuuza nishati hiyo.

Katika baadhi ya vituo vinavyouza mafuta hayo bei kwa sasa ni Sh. 4,000 hadi 5,000 kwa lita tofauti na elekezi ya ikiwa ni Sh. 2853 kwa petroli na Sh. 2,660 kwa dizeli kwa mkoa wa Songwe.

Mchungaji Haile Mwaijumba, mkazi wa Ihanda, wilayani Mbozi, aliyekutwa katika moja ya kituo cha mafuta, alisema tatizo la kukosekana kwa nishati hiyo limeleta usumbufu mkubwa na limejitokeza bila kupewa taarifa.

Dereva bodaboda, Mashaka Mwamlima, alisema anashangaa kuona vituo vya mafuta katika Mkoa wa Songwe vinakosa mafuta wakati juzi serikali ilitangaza kushusha bei ya bidhaa hizo.

Alisema hali hiyo imesababisha usumbufu mkubwa na watalazimika kusitisha biashara ya kubeba abiria kama hali ya kukosekana nishati hiyo itaendelea kwa muda mrefu katika mkoani humo.

Mmoja wa wauzaji mafuta ambaye ni msimamizi wa kituo cha kuuza mafuta cha Manyanya mjini Vwawa, wilayani Mbozi, Suke Ringa, alisema tatizo hilo limekuwa likijirudia kila mwaka inapofika miezi hii, huku akiainisha kuwa kwa sasa wauzaji wa mafuta wananunua kwenye 'Depot' moja pekee iliyopo jijini Dar es Salaam.

"Naomba watu wajue kuwa tatizo sio wafanyabiashara au matajiri zetu bali sijui tatizo ni nini kwani kila mwaka ikifika miezi kama hii kunaibuka tatizo la kukosekana kwa mafuta na hivi tunavyozungumza kuna depo moja tu inayouza mafuta huko Dar es Salaam hivyo inakulazimu kukaa muda mrefu kwenye foleni kupata mafuta," alisema Ringa.

Mmoja wa wauzaji wa mafuta, Jackson Haonga, alisema amelazika kuuza mafuta hayo kwa bei ya juu kutokana na kuadimika na namna anavyoipata kwa bei kubwa.

"Mafuta haya ni 'stock' (akiba) yangu niliyokuwa nikiipeleka kuuza kijijini, lakini baada ya kuona watu wanahangaika sana nimeamua kuuza hapa ili kuwahudumia wenzangu ambao wamekuwa wakihangaika," alisema.

**EWURA YAONYA**

Jana EWURA ilitoa taarifa ya onyo kwa baadhi ya kampuni za mafuta zinahodhi mafuta wakisubiri mabadiliko ya bei.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Dk. James Andilile, ilisema walipokea taarifa za uwapo wa baadhi ya kampuni za mafuta kuhodhi mafuta kwa ajili ya maslahi binafsi ya kibiashara ikiwamo kusubiri mabadiliko ya bei.

Pia, alisema zipo kampuni nyingine zinazodaiwa kupakia mafuta kutoka kwenye maghala pasipo kuyauza na nyingine kukataa kuuza mafuta hayo kwa wamiliki wa vituo wasio kuwa na ubia au mikataba nao.

"Kutokana na hayo, EWURA imepata taarifa ya kuchelewa kufikishwa kwa mafuta katika baadhi ya maeneo ya pembezoni mwa nchi na miji.

"EWURA inapenda kuwajulisha wananchi wote kuwa nchi ina mafuta ya kutosha katika maghala ya kuhifadhia mafuta na wakati huo huo meli zenye shehena ya mafuta kutoka nje ya nchi zinaendelea kuingia na kushusha mafuta kama kawaida chini ya uratibu Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA)," alisema Dk. Andilile katika taarifa yake.

"Mpaka Julai 14, mwaka huu, mafuta yote yaliyokuwapo nchini ni lita 169,853,692 za mafuta ya petroli, lita 209,641,670 za dizeli, na lita 34,588,002 za nafuta ya ndege yanayotosheleza mahitaji.

Alitoa onyo kwa kampuni za mafuta zinazohodhi mafuta na kuzitaka kuacha mara moja na kwamba kufanya hivyo ni kinyume cha sheria, kanuni zinazosimamia biashara ya mafuta nchini na masharti ya leseni zao za biashara.

"EWURA inapenda kuwataarifu wananchi kuwa itaendelea kufanya ukaguzi wa kina kwenye maghala na vituo vya mafuta na kuwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa wote watakaothibitika kukiuka sheria, kanuni na masharti ya leseni ikiwamo kuwanyang`anya leseni ya biashara kwa mujibu wa kanuni namba 6 ya kanuni ndogo za uokoaji wa bei za mafuta GN.57 ya mwaka 2022," alisema.

***Imeandikwa na Elizabeth Zaya (DAR) na Moses Ng'wat (Songwe)**

## HABARI KITAIFA

# Jecha afariki dunia, Samia amlilia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jecha Simai Jecha, amefariki dunia baada ya kuugua kwa muda mrefu.

Jecha alifariki dunia jana katika Hospitali ya Jeshi Lugalo mkoani Dar es Salaam alikokuwa anapatiwa matibabu na kuzikwa kijijini kwao Mkwajuni, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Jina lake lilipata umaarufu mkubwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 baada ya kufuta matokeo ya uchaguzi huo, kitendo kilichowakasirisha wafuasi wa vyama vya upinzani.

Ushindani mkubwa katika uchaguzi huo ulikuwa kati ya Dk. Ali Mohamed Shein wa CCM ambaye alikuwa akiomba ridhaa ya kuongoza Zanzibar kwa kipindi cha pili cha miaka mitano na mgombea wa CUF, Maalim Seif Sharif Hamad.

Baada ya kufuta uchaguzi huo, Jecha akiwa katika Televisheni ya Taifa ya Zanzibar (ZBC), alitangaza kurudiwa uchaguzi huo, uamuzi ambao uligomewa na CUF na wagombea wake wote kuanzia madiwani, wawakilishi na Rais hawakushiriki uchaguzi wa marudio.

Vyama vya upinzani vilimlaumu Jecha kwa kufuta uchaguzi huo ambao kwao waliamini ulikuwa huru na wa haki.

Kuanzia hapo, jina la Jecha lilikuwa mwiba mchungu kwa wapinzani. Ilifikia hatua kiongozi huyo kuongezwa ulinzi kazini hadi nyumbani.

Katika kinyang'anyiro cha kugombea urais wa Zanzibar 2020, Jecha alijitokeza kuchukua fomu kuwania uongozi kupitia CCM. Hata hivyo, jina lake halikurudi.

Jecha aliyezaliwa visiwani Zanzibar mwaka 1952, alihitimu elimu yake ya msingi mwaka 1966, na baadaye elimu ya juu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1977 na kupata shahada yake ya kwanza, Shahada ya pili aliipata Marekani katika Chuo cha New York.

Jecha kabla ya kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, aliwahi kuwa Kamishna wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

Pia aliwahi kuwa mwalimu wakati huo Maalim Seif akiwa Waziri wa Elimu na baadaye Waziri Kiongozi wa Zanzibar.

Aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Vuai Ali Vuai, anamzungumzia Jecha kama mtu hodari na mchapakazi aliyejitoa wakati wote kwa ajili ya nchi yake.

"Tumempoteza mtu muhimu na mzalendo wa kweli kwa nchi yake. Daima tumkumbuka kwa mema aliyofanya kwa Zanzibar," alisema Vuai.

Vuai ndiye alikuwa Katibu Mkuu wa CCM katika Uchaguzi Mkuu wa 2015 ambao ulisimamiwa na ZEC chini ya uenyekiti wa Jecha.

Aliyekuwa Mkurugenzi wa ZEC katika uchaguzi wa 2015, Salum Kassim Ali, alisema alifanya kazi na Jecha kwa karibu na alimpa ushirikiano uliohitajika.

"Aliishi vizuri na wafanyakazi na kila alipohitaji ushauri hakusita kufanya hivyo licha ya yeye kwa nafasi yake hakupasa kuomba," alisema.

Jana jioni, Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu, ilitoa taarifa kwa vyombo vya habari ikieleza kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ametuma salamu za rambirambi kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki kufuatia kifo cha Jecha.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya Ikulu, Rais Samia amepokea taarifa za kifo cha Jecha kwa majonzi na masikitiko. Pia ametuma salamu za rambirambi kwa familia ya aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa kufuatia kifo cha Bernard Mkapa ambaye alikuwa kaka yake.

"Rais Samia amewaomba wanafamilia wote wawe na moyo wa uvumilivu katika kipindi hiki kigumu cha majonzi na amewaombea marehemu wote wapumzike mahali pema peponi," ilibanisha taarifa ya Ikulu.




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania)**

TAARIFA inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni ya muda kuzalisha umeme kutoka kwa Kampuni ya Tangulf Nakatuta Energy Company Limited. EWURA inakaribisha maoni au pingamizi kuhusiana na maombi hayo ya leseni. Taarifa za mwombaji pamoja na aina ya leseni iliyoombwa zimetolewa hapa chini:

| Na. | MAELEZO |
|---|---|
| **Jina na anuani ya Mwombaji** | Tangulf Nakatuta Energy Company Limited, S.L.P 13412, Dar es Salaam. |
| **Eneo** | Kiwanja namba 12, Block A, Kata ya Muhurukuru, Wilaya ya Songea, Mkoa wa Ruvuma |
| **Taarifa za Wanahisa** | 1) Vetex Capital Limited, S.L.P 13412, Dar es Salaam, **0.14%.**<br>2) Tangulf Express Limited, S.L.P 22961, Dar es Salaam, **1.14 %.**<br>3) Said Rashid Kilahama, S.L.P 2269, Dar es Salaam, **0.14 %.** |
| **Maelezo ya Mtambo na Matumizi** | Kuzalisha umeme wa Megawati tano (5) kutumia maji kutoka maporoko ya mto Ruvuma. Umeme utakaozalishwa unategemewa kuuzwa kwa TANESCO |
| **Aina na Muda wa Leseni** | Leseni ya kuzalisha umeme kwa muda wa miaka mitatu (3) |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana na maombi haya awasilishe kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu siku ya kutolewa kwa tangazo hili. Maombi ya leseni yanaweza kuonyeshwa kwa mtu kwa maombi maalum ya maandishi.

**Mkurugenzi Mkuu**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go.tz

175039



## Lawyers' Environmental Action Team (LEAT) Publication of Bi-Annual Income and Expenditure

Lawyers' Environmental Action Team is a Non-Governmental Organization which was founded in 1994 and is registered under the NGOs Act of 2002 with (Certificate of Compliance No. 1985).

**Vision:** Tanzania with sustainable and well-managed environment and natural resources for current and future generations.

**Mission:** To contribute towards good governance in the use and sustainable management of the environment and natural resources through public interest litigation, advocacy, strategic research, capacity building, and networking.

In accordance with Non-Governmental Organization (Amendment) Regulation, 2018, Lawyers' Environmental Action Team (LEAT) is pleased to publish the amount of funds received and expended from January, 2023 to June 2023.

**Bi-Annual Income and Expenditure for the period from January 2023 to June 2023**

| **INCOME;** | **TZS.** |
|---|---|
| Receipt from Donors | 1,185,999,053.92 |
| **Total Income** | **1,185,999,053.92** |
| **EXPENDITURE ON PROJECTS;** | |
| Usimamizi Endelevu wa Maliasili | 827,517,459.11 |
| Advocacy for improved Legal and Regulatory regimes of Mineral and Petroleum laws in in Tanzania | 220,038,993.85 |
| Collective Action for Rights Realization in the Extractive Industry | 75,868,767.45 |
| Enhancing Protection of Environmental Defenders in Africa | 52,374,567.71 |
| Human & Admin Resources Activities | 10,199,265.80 |
| **Total Expenditure** | **1,185,999,053.92** |

In sum, LEAT received grants from the following donors: Open Society Initiative for Eastern Africa (OSIEA), United States Agency for International Development (USAID-Tanzania); America Bar Association (ABA) and VSO.

**Lawyers' Environmental Action Team (LEAT),**
**Mazingira House, Mazingira Street, Mikocheni B,**
**House No 8,**
**P.O. Box 12605, Dar es Salaam.**
**Email: info @leat.or.tz.**

217504102

# 500 watibiwa JKCI kila siku

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) imebainisha inatoa matibabu kwa takribani wagonjwa 500 kwa siku huku wanaolazwa kwa wiki wakifikia 130.

Vilevile, imebainisha kuwa kati ya wagonjwa hao wanaopokewa, baadhi hupatiwa huduma za upasuaji wa mishipa ya damu, mapafu na wa moyo kwa kufungua kifua.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumzia matarajio yao kwa mwaka 2023/24 ambao wamepanga kutumia Sh. bilioni 66.3.

Alisisitiza wananchi kuepuka magonjwa ya moyo kwa kuwa ni ghali. Alisema njia sahihi ya kuyaepuka ni kuwa na ratiba ya kufanya mazoezi na kuzingatia lishe sahihi.

"Ninaomba kuwakumbusha wananchi kuzingatia lishe bora kwa kula matunda, mboga za majani, vyakula vyenye madini ya potasium, kupunguza kula vyakula vyenye kiasi kikubwa cha mafuta na chumvi.

"Pia waepuke uvutaji wa sigara na unywaji wa pombe uliokithiri, kutambua kiwango cha sukari katika mwili wako, kutambua msukumo wako wa damu na kiwango cha mafuta mwilini. Kupima afya ya moyo walau mara moja kwa mwaka," alisema Dk. Kisenge.

Akieleza kuhusu huduma zilizotolewa mwaka wa fedha 2022/23 kwa kutumia bajeti ya Sh. bilioni 44.5, alisema zilijumuisha wagonjwa kuchunguzwa, kuzibuliwa mishipa ya damu ya moyo na kuwekewa vifaa visaidizi vya moyo.

Daktari Bingwa huyo alisema kwa kipindi hicho taasisi iliona wagonjwa 122,362. Kati yao, watu wazima ni 111,542 na watoto 10,820 huku wakilazwa 4,407. Kati ya hao waliolazwa, watoto ni 1,121.

"Wagonjwa waliofanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo wa kufungua kifua na kubadilishwa valvu za moyo moja hadi tatu, upasuaji wa kupandikiza mishipa ya damu ya moyo, upasuaji wa mishipa ya damu na mapafu walikuwa 714. Kati ya hao, watu wazima 412 na watoto 305," alisema Dk. Kisenge.

Kuhusu uchunguzi wa maabara kwa kutumia mionzi, Dk. Kisenge alisema wagonjwa 2,046 kati yao, watu wazima 1,762 na watoto 284, walipata huduma hizo na pia matibabu ya mfumo wa umeme wa moyo, mishipa ya damu ya moyo iliyokuwa imeziba na kuwekewa vifaa visaidizi vya moyo yalifanyika.

"Gharama ya matibabu ya wagonjwa hawa 2,760 tuliowafanyia upasuaji mkubwa na mdogo wa moyo kama wangetibiwa nje ya nchi ni Sh. bilioni 62.34, lakini kwa kutibiwa kwao katika taasisi yetu matibabu yao yamegharimu Sh. bilioni 31.17, fedha ambazo zimelipwa na bima za afya, ndugu wa wagonjwa, wafadhili na msamaha wa matibabu.

"Kwa kipindi cha mwaka mmoja wagonjwa waliotibiwa kutoka nje ya nchi walikuwa 301. Wagonjwa hawa walitoka katika nchi za Somalia, Malawi, Kenya, Rwanda, Uganda, Zambia, Visiwa vya Comoro, Ethiopia, Burundi na wengine kutoka nje ya Afrika, zikiwamo nchi za Armenia, China, India, Norway, Marekani na Uingereza," alisema.

Alisema kwamba taasisi hiyo ilitumia Sh. bilioni 1.249 kwa ajili ya kununua mashine mbalimbali, zikiwamo za kidigital, X-Ray na mashine tatu za kuangalia jinsi moyo unavyofanya kazi.

Bingwa huyo alisema Aprili mwaka huu, taasisi hiyo ilitia saini makubaliano ya miaka miwili na Hospitali za Taifa za nchi ya Rwanda na Zambia, kutoa matibabu kwa wagonjwa wa moyo pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wa afya wa hospitali hizo.

Alisema makubaliano mengine ni kushirikiana katika utoaji wa huduma za matibabu kwa wagonjwa, kubadilishana ujuzi wa kazi, kufanya utafiti na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa JKCI na chuo Kikuu cha Jagiellonian kilichopo Poland.

Pia Chuo cha Madaktari wa Upasuaji Afrika Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika (COSESCA) nchini Malawi, Taasisi ya Afya Ifakara (IHI), Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Alisema kwa mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Pwani, Arusha, Geita, Iringa, Mtwara, Lindi, Unguja, Manyara na Pemba wananchi 6,309 walifikiwa na huduma na kati yao, 3,239 walikutwa na matatizo ya moyo na waliopewa rufani kutibiwa JKCI walikuwa 724.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

## TANGAZO KWA UMMA

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemevu anakaribisha maombi ya vijana kujiunga na mafunzo kwa njia ya vitendo (Incubation) kuhusu utengenezaji wa vizimba vya samaki; utengenezaji wa boti za ute kioo (fibre boats); utengenezaji wa chakula cha samaki; ufugaji wa samaki kwenye vizimba; ufugaji wa majongoo bahari, unenepeshaji kaa na kilimo cha mwani; uchakataji wa samaki; uzalishaji wa vifaranga vya samaki pamoja na ujasiriamali yatakayogharamiwa na Serikali.

1. **Sifa za Mwombaji**
   i. Mwombaji awe kijana wa kitanzania mwenye umri usiopungua miaka kumi na nane (18);
   ii. Awe amehitimu fani za uvuvi na ukuzaji viumbe maji au mwenye nia ya kujishughulisha na uvuvi na ukuzaji viumbe maji;
   iii. Awe tayari kupata mafunzo kwenye mikoa na vituo vilivyoteuliwa; na
   iv. Awe tayari kujitegemea kwa malazi na chakula.

2. **Muda wa Mafunzo: -**

Mafunzo yatatolewa na Serikali kwa muda wa miezi mitatu (3) katika Mikoa ya kanda ya Ziwa Victoria na Pwani. Nafasi zilizopo kwa ajili ya mafunzo hayo ni **mia tatu (300)** tu. Aidha, Serikali itatoa **kiasi cha shilingi 150,000/= kwa kila mshiriki kwa mwezi.**

3. **Jinsi ya kutuma Maombi**
   i. Barua ya maombi iambatanishwe na nakala ya vyeti pamoja na wasifu (CV);
   ii. Maombi yote yatumwe kwa **Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, S.L.P 2847, Mji wa Serikali, Mtumba, Mtaa wa Ulinzi 40487-Dodoma** na kuwasilishwa kupitia barua pepe **barua@uvuvi.go.tz**
   iii. Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **09 Agosti, 2023 saa 9:30 Alasiri.**
   iv. Kwa maelezo zaidi wasiliana **0717 369 588/0655 669 942/0788 648 643.**

Imetolewa na:
**KATIBU MKUU**

175043

## Askari wa wanyamapori afariki dunia akivusha ng'ombe mtoni

**Na Halfani Chusi**

ASKARI wa Wanyamapori wa Hifadhi ya Taifa Ruaha (RUNAPA), Alphonce Ulomi (31), amefariki dunia baada ya kusombwa na maji ya Mto Ruaha wakati akivusha ng'ombe aliowakamata hifadhini eneo la Mbarali mkoani Mbeya.

Jana, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Anthony Mkwawa, akizungumza kwa niaba ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Benjamin Kuzaga aliyekuwa safarini, alithibitisha kuwapo tukio hilo.

Alisema kuwa askari huyo alifariki dunia Julai 15, mwaka huu saa saba mchana.

Alifafanua kuwa askari huyo alikuwa ameshikilia mkia wa ng'ombe wakati wa kuvuka mto huo. Aliteleza na kusombwa na maji.

Alisema kuwa baada ya kupata taarifa hizo, Julai 16 walianza kumsaka askari huyo na kuupata mwili wake huku silaha yake ikiwa shingoni.

"Walikuwa doria RUNAPA. Walikuwa askari watatu. Walikamata ng'ombe 170 waliokuwa hifadhini, baada ya kuona wafugaji wamekimbia ikabidi wawaswage kuwapeleka katika kambi kubwa Mkulanga.

"Wakati wanavuka katika huo mto, yeye (askari) alishika mkia wa ng'ombe ili wamsaidie kuvuka. Sasa bahati mbaya akawa ameuachia ule mkia, akadumbukia kwenye kina kirefu cha maji. Ilikuwa majira ya saa saba mchana. Baada ya hapo kesho yake (siku iliyofuata) alipatikana.

"Mwili wake umeagwa leo (jana) Iringa na anakwenda kuzikwa nyumbani kwao mkoani Kilimanjaro," alisema ACP Mkwawa.

Kuhusu walioingiza mifugo hifadhini, kiongozi huyo Jeshi la Polisi alisema kesi ilishafunguliwa na wahusika watapelekwa mahakamani hivi karibuni baada ya upelelezi kukamilika.

Alipotafutwa kwa njia ya simu mmiliki wa ng'ombe waliochukuliwa, Waziri Msangu alithibitisha ng'ombe wake 170 wako chini ya uangalizi wa hifadhi tangu walipochukuliwa hifadhini.

"Kwa sasa ninasubiri hukumu ya mahakama ili niweze kulipa faini, nipate mifugo yangu. Ninachoomba wasiipige mnada, bora waniambie nilipe faini kwa kuwa nipo tayari kwa hilo," alisema.

**RIPOTI YA UCHUNGUZI**

# Karata za Mbuga ya Wanyama Saadani

**Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa**
BAGAMOYO

JARIBU kukumbuka kauli hii ya Oktoba 6, 2016 kutoka Mkuranga, mkoani Pwani: "Tena ndugu yangu... nitakupa eneo ulime miwa ili upate sukari ya viwandani na ya majumbani, tena nitakupa bure."

Huyo ni Rais John Magufuli akizindua kiwanda cha kusindika matunda na kuzalisha juisi cha Bakhresa Food Products Ltd kilichoko Mwandege wilayani Mkuranga, mkoani Pwani.

"Wewe Bakhresa umenifurahisha sana kwa uwekezaji wako; na sukari yako niliyoizuia bandarini, leo (Oktoba 6, 2016) ninamwagiza Waziri (Charles) Mwijage itoke na upatiwe."

Kauli hiyo ilikuwa ikitoa idhini kwa Bagamoyo Sugar Limited (BSL), kampuni tanzu ya Said Salim Bakhresa (SSBG), kupata ardhi katika Mbuga ya Wanyama ya Saadani, mkoani Pwani.

Hata hivyo, wakati Rais Magufuli anatangaza kutoa ardhi kwa BSL, mwandishi amegundua, hatimiliki Na. 156361MG ya kutwaa eneo mbugani Saadani iliishaandaliwa - tangu tarehe 1 Oktoba 2016. Hati ilitangulia ahadi!

Je, inawezekana rais alikuwa hajui sheria na kanuni zinazotawala mbuga za wanyama?

Kanuni Na. 9 ya Kanuni 15 za Usalama za Hifadhi ya Taifa Saadani (SANAPA), inapiga marufuku upandaji mmea wowote ndani ya mbuga hiyo.

Lakini hadi sasa, wazalishaji sukari wameshapanda miwa katika hekta 2,000 kati ya hekta 10,000 walizomegewa hifadhini: Namba ya usajili: 3565-1 na umiliki wa miaka 66.

Msemaji wa Kampuni za Said Salim Bakhresa (SSBG), Hussein Sufian, ambao kiwanda cha sukari ni kampuni yao tanzu, amemwambia mwandishi wa habari hizi kuwa wao walipatiwa eneo hilo kupitia uamuzi binafsi wa Rais John Magufuli na wala hawakuomba eneo hilo.

Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009 na Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura 282 (2002), zinazuia kujenga kiwanda na kufanya shughuli zingine za binadamu katika hifadhi za taifa. Lakini BSL imeshajenga kiwanda na inazalisha sukari ndani ya Mbuga ya Saadani.

Utata katika hili ni kwamba, mtoa leseni ya uwekezaji huo mbugani ni serikali - mara hii, hata kwa nguvu ya nyongeza ya kauli ya rais aliyekuwa madarakani.

Vilevile, mmiliki wa Mbuga ya Saadani ni serikali na msimamizi wa utekelezaji wa sheria zinazozuia shughuli kinzani hifadhini ni serikali. Je, serikali au watendaji wake wanafanya makusudi kuvunja sheria na kanuni za hifadhi ya Saadani?

Msemaji wa mwekezaji - SSBG, Hussein Sufian, katika mazungumzo na mwandishi Juni 19 mwaka huu, alisema, "Shida iliyopo ni suala la mpaka. Wizara ya Ardhi wanasema ni wamiliki wa eneo hilo. Wizara ya Maliasili na Utalii wanasema jiwe la mpaka (GN) la hifadhi limepita katika eneo hilo (lao)."

"Sisi (SSBG) hatukuomba eneo (hili). Tulipewa na Rais na akaagiza tulime miwa na kuzalisha sukari," Sufian anasema bila shaka, bila ufahamu wa hoja kuu ya kulinda na kuhifadhi ikolojia ya anakotifua na kuzamisha mbolea yenye kemikali ambazo wataalamu wanaonya huenda zikawa hatarishi kwa viumbe mbugani.

Ardhi walikopewa BSL inahusisha maeneo matano kati ya manane muhimu kwa ikolojia ya SANAPA. Baadhi ya maeneo hayo sasa yanatumika kwa kilimo cha miwa ambayo ni malighafi ya kiwanda cha sukari.



Kinachosikitisha ni kwamba, miaka yote maeneo yaliyotwaliwa kwa kilimo cha miwa, yamekuwa yakitumiwa na wanyamapori kuzaliana. Mengine yamekuwa njia maalum za wanyama (ushoroba), vyanzo vya maji ya Mto Wami na mlango wa maji wanayokunywa.

Vilevile, eneo lililomegwa kwa ajili ya mradi wa kilimo cha miwa na kiwanda cha sukari, lina msitu wa mikoko inayotumika kudhibiti uchafuzi wa mazingira. Eneo hili pia, ni mazalia ya kasa wa kijani - viumbe walio hatarini kutoweka duniani.

Aidha, eneo ililopewa kampuni hiyo ndilo limekuwa linategemewa na wanyamapori kupata maji na malisho wakati wa kiangazi kutokana na asili yake ya kijani kibichi.

Ramani iliyopo inaonesha eneo la hifadhi hiyo linajumuisha Mto Wami, ambao ni maarufu kwa utalii wa boti ili kuona mamba na viboko.

Mbali na kulindwa na Sheria ya Hifadhi za Taifa na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori kwa kuwa umo ndani ya Hifadhi ya Taifa, Mto Wami unalindwa na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004, inayozuia kufanya shughuli za binadamu ndani ya eneo la mita 60 toka ukingo wa mto.

Kifungu cha 57(1) cha sheria hiyo kinaelekeza: "Ndani ya mita sitini (60) hakutafanyika shughuli yoyote ya binadamu ya kudumu au ambayo kwa asili inaweza kuhatarisha au kuathiri vibaya ulinzi wa mazingira na, au utunzaji wa bahari au kingo za mto, bwawa, au miambao ya asili ya ziwa."

Haya yote hayakuzingatiwa wakati wa kugawa eneo la Saadani kwa wawekezaji wa kilimo na kiwanda cha sukari - wagawaji wakiwa serikali iliyotunga sheria na kanuni za hifadhi za mbuga za wanyama.

Mwezi Aprili mwaka huu, mwandishi wa habari hizi alihojiana na aliyekuwa Mkuu wa SANAPA, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi Ephraim Mwangomo juu ya utata huu ambaye alikuwa na maoni haya:

"Bagamoyo Sugar Limited hawana kosa. Makosa yako kwa watendaji wa serikali kutoa kibali cha shughuli za aina hii (kilimo cha miwa na uzalishaji sukari) hifadhini.

"Wao (Bagamoyo Sugar Limited) wamepewa eneo na serikali walime miwa na kuzalisha sukari kiwandani."

Kamishna Mwangomo, ambaye mwezi Mei mwaka huu alihamishwa SANAPA kwenda kuwa Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, alitaja shida nyingine iliyoko katika eneo hilo kuwa ni kutokuzingatiwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 wakati wa kumpata mwekezaji na kumega eneo.

Anafafanua, "GN ya hifadhi inajumuisha Mto Wami unaolindwa na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Sasa lazima kuwe na utii wa Sheria ya Mazingira.



Tembo walipopita katika shamba la miwa la BSL wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani hivi karibuni **PICHA: SANAPA**

"Shida nyingine ni kwamba, tembo wanapenda mno miwa. Kulima miwa hifadhini au karibu na eneo lenye tembo ni kuwatia tembo majaribuni 'for no reason' (bila sababu). Lile eneo ni 'part and parcel of their eco-system' (ni sehemu ya mfumo wao wa kiikolojia)," Kamishna Mwangomo alisema.

Mhifadhi huyo aliongeza, "Tembo wakishaingia katika shamba la miwa, kwa saa chache tu wanakula miwa mingi, wanaharibu eneo kubwa. Mara nyingi wanatembea wakiwa kundi kubwa. Wale wenye mradi (BSL) wakishawaona tembo, wanatuita, tunawasaidia kuwaswaga.

"Lakini tukumbuke, tembo ni miongoni mwa wanyamapori wenye akili nyingi. Tayari wameshabaini kwamba wakiingia shambani mchana, ni rahisi kushtukiwa. Wamebadili utaratibu, sasa wanaingia shambani usiku."

SANAPA ina tembo 359 kwa mujibu wa Sensa ya Wanyamapori ya Mwaka 2022.

Kuhusu jinsi ya kumaliza utata huu, Msemaji wa SSBG, Sufian, anasema, wamekuwa na majadiliano na makatibu wakuu wa wizara hizo (Wizara ya Ardhi na Wizara ya Maliasili na Utalii) tangu miaka mitatu iliyopita.

Anasema serikali, katika kusaka utatuzi wa mvutano huo, iliwataka wasalimishe eneo la mita 500 kutoka ukingo wa Mto Wami kama ilivyoopendekezwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kwa ajili ya uendelevu wa ikolojia ya Hifadhi ya Saadani.

Hata hivyo, msemaji huyo amesema badala ya kutekeleza hilo, wamekuja na makubaliano mapya yaliyofikiwa na pande hizo mbili; kuwa wazalishaji sukari wasalimishe eneo la mita 200 kutoka ukingo wa Mto Wami na kwa upande wake serikali isalimishe mita 300.

Taarifa za hatua hii ya makubaliano zimethibitishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2021/22. Ripoti hiyo iliwasilishwa bungeni Aprili 6 mwaka huu.

Kuhusu maendeleo, Msemaji wa SSBG amesema katika msimu uliopita, walizalisha tani 18,500 za sukari kutoka hekta 1,200 zilizoendelezwa; kazi iliyofanywa na watumishi 120 wa kudumu na 45 wa msimu. Amesema msimu ujao wanatarajia kuzalisha kati ya tani 35,000 na 40,000 za sukari.

Kwa mujibu wa Sufian, malengo ya kimkakati yaliyopo kwa kampuni hiyo itakapoingia awamu ya tatu ya mradi wake, ni kuzalisha tani 100,000 za sukari kwa mwaka.

Kampuni imewekeza dola za Marekani milioni 110 (Sh. bilioni 265.678) na katika awamu ya tatu, anaeleza Sufian, watapanua uwekezaji hadi dola milioni 300 (Sh. bilioni 724,575). Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21, CAG Kichere, alipendekeza serikali na TANAPA kufanya tathmini ya kina kuhusu uhalali na athari za uendeshaji wa mashamba ya miwa na kiwanda ndani ya Hifadhi ya Saadani.

Vilevile, alipendekeza kutafutwe njia bora ya kukabiliana na hali hiyo. Matokeo ya tathmini yawe marejeo kwa matumizi ya baadaye.

Wataalamu wa uhifadhi na utetezi wa ikolojia pamoja na wanaharakati, wanaendelea kupinga shughuli zozote za binadamu katika mbuga za wanyama na ukiukwaji wa sheria na kanuni za uhifadhi wa mazingira.

***FUATILIA KESHO MADHARA YA KILIMO NA UENDESHAJI KIWANDA HIFADHINI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utaratibu kuwezesha hoteli kubadili fedha utasaidia

**KATIKA** kurahisisha utoaji wa huduma ya kubadili fedha za kigeni, Benki Kuu ya Tanzania (BoT), imeamua kuanzisha kanuni mpya zinazolenga kuweka utaratibu utakaowezesha hoteli za kitalii nchini kutoa huduma ya kubadilisha fedha za kigeni kwa wateja wao.

Hatua hiyo imetokana na hoteli hizo kupokea idadi kubwa ya wageni ambao wanafanya malipo kwa fedha za kigeni ambao utaiwezesha serikali kujua takwimu sahihi za fedha za kigeni.

Akizungumza na wadau wa biashara ya ubadilishaji fedha juzi, Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, amefafanua kuwa BoT kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ilikutana na wadau wa sekta ya hoteli Zanzibar, Januari mwaka huu na kujadili namna ya kuboresha upatikanaji wa huduma ya kubadilisha fedha za kigeni katika maeneo ya hoteli za kitalii.

Hatua hiyo inatokana na BoT kubaini kwamba wamiliki wa hoteli wanapokea fedha nyingi za kigeni kupitia wageni wanaofanya malipo ya kulala, hali inayoinyima serikali kufahamu takwimu sahihi za fedha za kigeni.

Benki hiyo imebaini kuwa mmiliki wa hoteli akipokea fedha za kigeni anakwenda kuzibadili ili alipe mishahara, anunue bidhaa na kwa kuanzisha kanuni mpya, mmiliki wa hoteli akishapokea fedha hizo atatakiwa kuzisajili, atatoa taarifa kwa serikali, kisha atazieweka kwenye akaunti yake ya benki na serikali itaziona.

Lengo la hatua hizo ni kujua takwimu za fedha za kigeni zinazoingia nchini.

Hata hivyo, BoT inaendelea kuhamasisha benki na taasisi za fedha kuboresha utoaji wa huduma ya kubadilisha fedha za kigeni na kwamba hadi Juni mwaka huu benki za bishara 37 zenye mtandao wa matawi zaidi ya 900 yaliyosambaa nchi nzima yameendelea kutoa huduma hizo.

Maduka ya kubadilisha fedha manane yenye matawi 36 nchini yalikuwa yamepewa leseni.

Kadhalika, BoT imetaja sababu za kuadimika kwa Dola ya Marekani nchini kuwa ni kuongezeka kwa mahitaji ya fedha hiyo kutokana na uchumi kufunguka baada ya janga la ugonjwa wa Uviko.

Sababu nyingine iliyosababisha dola kuadimika ni vita kati ya Urusi na Ukraine ambayo imepandisha bei za bidhaa na huduma mbalimbali ikiwamo usafirishaji na kuongeza mahitaji ya dola.


Vile vile, mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha mahitaji makubwa zaidi ya dola pamoja na sera ya fedha ya Marekani (kupandisha riba) iliyovutia wawekezaji wengi kuwekeza Dola zao Marekani na kusababisha uhaba duniani.

BoT imeendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa upatikanaji wa dola na sarafu nyingine na kigeni na kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi hauathiriwi sana na changamoto hiyo.

Hata hivyo, BoT imewahakikishia Watanzania kuwa licha ya changamoto hiyo ya kidunia, Tanzania imeendelea kuwa na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi isiyopungua minne.

Mpaka Julai 14, mwaka huu akiba ya fedha za kigeni ilikuwa ni Dola za Marekani bilioni 5.55, ambayo inakidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kwa takriban miezi mitano.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Kujifunza ughaibuni kunufaishe wengi

**WADAU** na serikali wanafanya kila mbinu kuandaa kizazi cha vijana watakaoweza kutambua fursa na kuzitumia ili kubadilisha maisha yao.

Eneo mojawapo ni kilimo na ufugaji ambalo serikali na wadau wameanza uwekezaji mathalani, kwenye mradi wa mafunzo ya vitendo kwa vijana walio katika mpango wa "jenga kesho iliyobora" Building Better Tomorrow (BBT), unaoendelea jijini Dodoma.

Katika kuunga mkono juhudi za serikali wadau wa Shule ya Sekondari ya Imperial iliyoko Chalinze mkoani Pwani, inapeleka wanafunzi kujifunza kilimo cha kisasa Misri na Israel.

Ikiwa ni moja ya masomo yanayofundishwa shuleni hapo, uongozi umeamua kuwapa elimu zaidi kwa vitendo kupitia ziara hiyo ya mafunzo Misri na Israel, mataifa yenye ushawishi na utaalamu mkubwa kwenye kilimo na ufugaji.

Ziara inalenga kuwagusa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita wanaotarajiwa kujifunza kwa siku 10 na kurudi na maarifa, kama anavyoeleza Ahmed Salim, mwalimu na mkuu wa msafara huo.

Wanafunzi hao 30 kutoka kidato cha kwanza hadi cha sita, wanatarajiwa kujifunza kilimo na ufugaji wa kiteknolojia.

Ni ili wapate elimu ya vitendo baada ya kujifunzi ile ya nadharia darasani na kuwajengea uwezo waweze kujitegemea na kuwa wataalamu na wawekezaji siku zijazo.

Pamoja na kilimo na ufugaji wanafunzi hawa wanapelekwa pia kujifunza teknolojia na ubunifu kwenye viwanda, ziara ikiwafikisha kwenye kiwanda kidogo kilichoko Cairo kinachotumia teknolojia nyepesi kutengeneza karatasi za kuchorea cha New Abu Simbel Papyrus.

Mwalimu Salim anasema katika eneo hilo wanajifunza mimea mbalimbali inayotumika kutengenezea karatasi na mbinu za kuichakata.

Anataja magugu maji ambayo yamejaa kwenye vyanzo vingi vya maji nchini, lakini pia kuna teknolojia ya kutumia karatasi hizo kama taa sehemu zisizo na umeme, na kwamba mafunzo hayo yanalenga kuwapa nuru zaidi.

Akizungumzia ziara hiyo, mmoja wa wanafunzi, anasema ni muhimu kwani inawezesha kujifunza zaidi kilimo, biashara na ufugaji kwa kutumia teknolojia ya kisasa katika mnyororo wa thamani.

Wanategemea kurudi na ujuzi na maarifa ili kusaidia wenzao na taifa pia katika sekta mbalimbali ikiwamo kilimo na ufugaji.

Wanafunzi wanaamini kuwa itawawezesha kuwa na mawazo mapana, kuona fursa na kuzichangamkia ndania ya jamii, lakini kujiajiri, kuinua uchumi wa taifa na wa familia na ule wa mtu binafsi.

Utaratibu huo ni bora na shule nyingine pia zinatakiwa kuona fursa ya kuwapa watoto kama ikiwezekana ziara za kimasomo nje na hata ndani ya nchi ili kupanua zaidi uelewa na mawazo hasa baada ya kujifunza kwa vitendo.

Kujifunza kunaongeza nguvu na kuimarisha dhana ya uthubutu, kusaidia kuondoa hofu, woga na kufikiria kuwa jambo analotaka kuliendea ni gumu.

Lakini, mambo hayaishi hapo maana ni mafanikio kitaaluma kama wanafunzi wanapata nafasi ya kujifunza maarifa ya maendeleo, kiteknolojia katika umri mdogo hivyo hata wakiendelea vyuoni na vyuo vikuu wanakuwa na ufahamu wa kufanya uamuzi na kuendeleza sekta mbalimbali kwa maarifa na juhudi zaidi.

Licha ya kwamba sekondari hiyo imeanzishwa kwa malengo ya kutengeneza na kuandaa vijana wa kuendana na karne ya 21 ambayo inawajenga watoto wawe viongozi bora, wajiajiri, wasisubiri ajira, wawe na ujuzi na maarifa ya kupambanua mambo ni suala ambalo vyuo na shule nyingine inapendeza kulifikiria.

Ni vyema pia kuwa na ushirikiano wa kimasomo na mataifa na vyuo mbalimbali nje na ndani ili kuwapa nafasi wanafunzi wa Tanzania kuona dunia katika mwanga bora zaidi kwa kujifunza kwa vitendo yale ambayo yataamsha ari mpya ya kusoma na kuwa shujaa au mbobezi kwenye eneo mwanafunzi analolimudu.

# Mbaroni tuhuma kuoa mwanafunzi

## ●Wazazi wakimbia makazi kisa msako wa polisi

**Na Moses Ng'wat,** MBOZI

JESHI la Polisi mkoani Songwe linamshikilia Lukia Magwaza (21), mkazi wa Kijiji cha Shasya, Kata ya Halunga wilayani Mbozi kwa tuhuma za kumwoa mwanafunzi (jina limehifadhiwa) aliyetakiwa kujiunga na kidato cha tano.

Mwanafunzi huyo ambaye naye anashikiliwa na jeshi hilo, alihitimu kidato cha nne mwaka 2022 katika Shule ya Sekondari ya Spring Valley iliyoko mkoani Iringa na alitakiwa kujiunga na kidato cha tano baada ya kupata ufaulu wa daraja la tatu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Theopista Mallya, aliwaambia waandishi wa habari mjini hapa jana kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa usiku wa Julai 16, mwaka huu kwa ushirikiano kati ya jeshi hilo na uongozi wa kata.

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi alisema wanamshikilia mwanafunzi huyo kwa uchunguzi zaidi kwa kuwa baada ya kuhojiwa, alidai hajui kama alichaguliwa kuendelea na masomo kujiunga na kidato cha tano.

"Mtuhumiwa na mwanafunzi wote wamekamatwa. Wako kituoni kwa mahojiano zaidi, kwani mwanafunzi anadai alimaliza kidato cha nne na kufaulu kwa kupata daraja la tatu, lakini mpaka sasa hajui kama alichaguliwa kujiunga na kidato cha tano," alisema.

Kamanda Mallya aliongeza kuwa jeshi hilo linaendelea kuwatafuta wazazi wa pande zote mbili ambao wametoroka baada ya kubaini wanatafutwa kwa tuhuma za kushiriki kupanga ndoa hiyo.

"Kuna mazingira ambayo yanaonyesha wazazi wa pande zote mbili walibariki mpango wa ndoa hiyo na baada ya kujua kuwa vyombo vya dola vimebaini, wameamua kutorokea kusikojulikana," alisema Kamanda Mallya.

**"Mtuhumiwa na mwanafunzi wote wamekamatwa. Wako kituoni kwa mahojiano zaidi, kwani mwanafunzi anadai alimaliza kidato cha nne na kufaulu kwa kupata daraja la tatu, lakini mpaka sasa hajui kama alichaguliwa kujiunga na kidato cha tano," alisema.**



Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) Taifa, Mary Chatanda (wa pili kulia), akipata maelezo ya mradi wa kuchomea taka alipotembelea Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi juzi. Wa nne kulia ni Mkuu wa wilaya hiyo, Mohamed Moyo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Serikali yawapa angalizo wawekezaji kuhusu ardhi

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imewataka wawekezaji kuacha tabia ya kwenda kuchukua ardhi moja kwa moja kwa wananchi bila kupitia Kituo cha Uwekezaji (TIC), ili kuepuka migogoro inayoweza kutokea baina yao na wananchi.

Angalizo hilo lilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Ardhi Mwandamizi wa Wizara ya Ardhi, Dawati la Ardhi ya Uwekezaji Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani, Twahil Bishanga.

Alikuwa anazungumza katika mjadala wa pamoja kati ya Kundi la Wawekezaji wa Bara la Ulaya wapatao 50 na maofisa kutoka TIC na taasisi mbalimbali za serikali.

Walikutana kujadiliana kuhusu huduma za pamoja za uwezeshaji kwa wawekezaji na wafanyabiashara wanaotoka Ulaya zinazotolewa na TIC zilizopewa jina la 'One Stop Facilitation Services for European Businesses'.

Alisema baadhi ya wawekezaji wamekuwa na tabia ya kwenda kuzungumza na wananchi na kupewa ardhi bila kupitia TIC, jambo ambalo linaweza kuwasababishia usumbufu mkubwa siku za baadaye.

Alisema TIC ndio wanajua ardhi iliyotengwa maalum kwa wawekezaji na ambayo imewekwa miundombinu ya msingi kama maji, barabara na umeme, hivyo kuwa rahisi kwa mwekezaji kuanza uwekezaji mapema.

"Changamoto tuliyonayo ni wawekezaji wanapotaka ardhi kwenda moja kwa moja kwa wananchi kununua ardhi bila kushirikisha mamlaka zinazoratibu masuala ya uwekezaji. Madhara yake ni kwamba mara nyingi miradi wanayotaka kuweka inakinzana na matumizi ya ardhi ya maeneo waliyochukua.

"Kwa hiyo tumewashauri kwamba ni busara kabla ya kununua hayo maeneo waende TIC na EPZA ili kuoanisha kama miradi wanayotaka kuwekeza inakubalika kwa matumizi ya ardhi yaliyopangwa katika maeneo hayo," alisema.

Aliongeza kuwa kuna faida nyingi za kuchukua ardhi ambayo imeidhinishwa na TIC kwa kuwa inakuwa rahisi kwa serikali kupeleka miundombinu muhimu kama ya umeme, maji na barabara.

Mkurugenzi wa Kampuni ya European Business Group (EUBG), Emma Urio, alisema kampuni hiyo inawakilisha wawekezaji na wafanyabiashara 125 wanaotoka Bara la Ulaya wanaotoka sekta mbalimbali kama kilimo, viwanda na biashara.

Alisema lengo la kufanya mkutano huo ni kuleta ukaribu kwa wafanyabiashara wa Bara la Ulaya ili waelewe kuhusu huduma za One Stop Facilitation Center ya TIC na faida zake.

Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe De Boer, alisema wawekezaji hao wamefurahia mjadala uliofanywa kwa pamoja na maofisa wa serikali kuhusu huduma za pamoja kwa wawekezaji wanaotoka Bara la Ulaya.

Alisema wamepata maelezo kutoka taasisi 11 zinazofanya kazi kwa karibu na TIC kuhusu huduma ambazo wanaweza kuzipata kwa pamoja na kurahisisha uwekezaji tofauti na miaka ya nyuma.

"Uwazi wa kufanya kazi kwa taasisi za umma unafurahisha wawekezaji na wameendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini na rekodi zinaonyesha wawekezaji wanaendelea kuja kutokana na mazingira mazuri ya uwekezaji," alisema.

Mkurugenzi wa Uwekezaji wa TIC, John Mmari, alisema lengo la mkutano huo ni kuwakutanisha wawekezaji hao kutoka Ulaya na maofisa wa taasisi za serikali wanaotoa huduma za pamoja.

"Hawa wawekezaji wa Ulaya wana umoja wao hapa unaoitwa EUBG. Tulitaka wazifahamu huduma za pamoja zinazotolewa na taasisi zetu ili wanapopata changamoto wajue ni ofisa gani waende, TIC atatatua shida yake.

"Mkutano umekuwa mzuri, wameuliza maswali mengi na wamepewa ufafanuzi mzuri," alisema Mmari.

Alisema wawekezaji wamekuwa wakipata huduma mbalimbali kama vibali vya kuishi na leseni za uwekezaji wanapoingia nchini na huduma hizo huwa endelevu wanapoendelea kuwapo nchini wakifanya biashara mbalimbali.

"Kwa mfano vibali vya kazi huwa vinahitaji kuhuishwa kila baada ya muda fulani, kwa hiyo huduma kama hizo zinatolewa hapa pamoja.

"Lengo lingine la kuwakutanisha ni kuwapa nafasi ya kuzifahamu fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo," alisema.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



UHABA MIUNDOMBINU

# Wanafunzi wasomea nje, waketi sakafuni

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

SHULE ya Msingi Mukimbii, Kata ya Msange, Halmashauri ya Wilaya ya Singida, inakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa na madawati, hivyo kusababisha baadhi ya wanafunzi kuketi sakafuni na wengine kusoma nje ya vyumba vya madarasa.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Ally Sidet, alibainisha hayo alipotoa taarifa fupi ya shule hiyo wakati wa kupokea mradi wa maji safi, kiwanja cha michezo na bustani ya mboga kutoka kwa kiongozi wa shirika lisilokuwa la kiserikali la World Serve International Tanzania.

Alifafanua kuwa, kutokana na upungufu wa vyumba viwili vya madarasa uliopo kumechangia baadhi ya wanafunzi kusomea nje na upungufu wa madawati umesababisha wanafunzi kukaa chini na wengine kukaa kwa kubanana.

Alilitaja ni jambo linalosababisha wanafunzi kupata shida na kushindwa kupata masomo yao kikamilifu.

Mwalimu wa madarasa ya awali shuleni huko, Priscus Eliasi, alisema wazazi na walezi wa wanafunzi wa shule hiyo wana mwitiko mkubwa kwa kuwa ndiyo walioanza kujenga majengo ya shule hiyo kwa nguvu zao na ndipo serikali nayo ikaingiza mchango wake.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Elia Digha, alisisitiza kuwa ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa na madawati, ameliomba Shirika la Water Fund liwajengee vyumba viwili vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa madarasa ya awali.

Akizungumza kwa niaba ya shirika, Mkurugenzi wa World Serve Internatinal Tanzania, Simeon Vomo, alizitaja shughuli walizofanya katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida kuwa ni pamoja na kufunga mfumo wa maji katika Zahanati ya Mughunga, mfumo wa kuchuja maji katika Kijiji cha Msange na wana miradi 54 ya maji inayofanya kazi.

Ripoti ya Ukaguzi Maalum wa Miundombinu na Samani katika Shule za Msingi Tanzania iliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ilibaini shule nyingi zina hali mbaya katika eneo hilo.

CAG aliitaka serikali kujenga miundombinu mipya na kuiboresha iliyopo.




Wanafunzi 30 wa Shule ya Imperial ya Msolwa Chalinze mkoani Pwani, wakiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam juzi, kabla ya kuondoka kuelekea nchini Misri na Israel kwa ajili ya kujifunza kilimo na ufugaji wa kisasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dereva bajaji mbaroni tuhuma kunajisi watoto

**Na Moses Ng'wat,** SONGWE

JESHI la Polisi Mkoa wa Songwe linamshikilia dereva bajaji, Ayubu Mng'osi (30), mkazi wa Ichenjezya wilayani Mbozi kwa tuhuma za unajisi na shambulio la aibu dhidi ya watoto wawili wenye umri wa miaka saba na tisa ambao ni wanafunzi wa shule ya msingi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Theopista Mallya, alisema kuwa katika tukio la kwanza, mtuhumiwa huyo anadaiwa kumwingilia kimwili mwanafunzi wa darasa la nne katika shule ya msingi Ichenjezya (jina limehifadhiwa).

"Mbinu aliyotumia mtuhumiwa ni kumlaghai mtoto na kuingia naye ndani ya nyumba anayoishi ambako ni jirani na wazazi wa mtoto kisha kutekeleza unyama huo," alisema Kamanda Mallya.

Kamanda Mallya alisema mtuhumiwa huyo pia anadaiwa kumfanyia shambulio la aibu la kumshika na kumchezea sehemu za siri mtoto mwingine ambaye ni mwanafunzi wa darasa la pili katika shule ya Ichenjezya (jina limehifadhiwa).

"Julai 14 mwaka huu, huko katika maeneo ya Mianzini, Kata ya Ichenjezya, Frida Pasokoni, aligundua kushikwa, kuchezewa na Ayubu sehemu za siri maeneo ya makalioni kwa mjukuu wake mwenye umri wa miaka saba, mwanafunzi wa darasa la pili," alisema Kamanda Mallya.

Aliongeza kuwa uchunguzi wa awali unaonyesha mtuhumiwa huyo amekuwa anahusishwa na vitendo hivyo kwa nyakati tofauti na mbinu alizotumia ni kuwaingiza watoto hao ndani kwake na kuwafanyia vitendo hivyo.

Kamanda huyo alisema jeshi linaendelea kumshikilia mtuhumiwa na upelelezi utakapokamilika atafikishwa mahakamani kwa hatua za kisheria.

## RC awapongeza polisi kumbaini anayedaiwa kutaka kuchoma soko

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amelipongeza Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam kwa kushirikiana na wananchi kubaini mtu anayedaiwa kutaka kuchoma moto Soko la Mchikichini.

Vilevile, amewataka wafanyabiashara katika soko hilo kuwa walinzi namba moja wa eneo hilo.

Chalamila, baada ya kutembelea soko hilo jana akiambatana na Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alitoa onyo kwa wafanyabiashara wasio waaminifu ambao huunguza masoko kwa sababu zao binafsi.

"Nisisitize kwamba biashara ndiyo msingi wa maisha yenu, hivyo ninapenda kuwakemea watu wanaoleta chokochoko na kuhatarisha amani ya Dar es Salaam kwamba hapa si mahali pake," alionya.

Chalamila alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashairi ya Jiji la Dar es Salaam kuipatia ufumbuzi changamoto ya choo baada ya wafanyabiashara kueleza kwake kero hiyo, naye akisisitiza itatatuliwa.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema jeshi limeimarisha mifumo ya kiintelijensia kubaini watu waovu ili kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara saa 24.

Alisisitiza wafanyabiashara kuendelea kufanya biashara zao ili kuinua uchumi wao na taifa kwa ujumla.

## SBL yaja na kampeni uwezeshaji kiuchumi

**Na Halfani Chusi**

KAMPUNI ya Serengeti Breweries Limited (SBL) imezindua kampeni yake ya kitaifa ya 'Jibambe Kibabe' inayolenga kuchochea uwezeshaji kiuchumi katika mfumo wake wa biashara.

Chini ya kampeni hiyo, SBL itatoa motisha, marejesho ya fedha na punguzo kwa washirika wake wa biashara wanaponunua bia na vileo vyake.

Uongozi wa kampuni hiyo umesema washindi wa kampeni ya 'Jibambe Kibabe' kutoka mtandao wa biashara wa SBL ni pamoja na wauzaji wakubwa, wauzaji jumla, wasambazaji na maduka ya rejareja.

Kampeni hiyo ilizinduliwa rasmi jana katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika makao makuu ya kampuni hiyo mkoani Dar es Salaam.

Irene Mutiganzi, Mkuu wa Idara ya Vileo wa SBL, alisema kuwa kampeni hiyo inalenga kuwawezesha washirika wa kibiashara wa SBL, hasa katika mazingira ya uchumi ya sasa ambapo biashara zinakaribia kupona kutokana na kutokuwa na uhakika wa kiuchumi.

Mutiganzi alieleza kuwa katika miaka iliyopita, kama ilivyo kwa biashara zingine nyingi, SBL na washirika wake wa biashara wamekabiliana na changamoto kutokana na mazingira ya kiuchumi ya kimataifa yanayojitokeza.

Akifafanua kuhusu muundo wa kampeni hiyo, Mutiganzi alisisitiza kampeni inawapatia wateja wanaofanya vizuri punguzo na marejesho ya fedha, na pia kuwapa fursa ya kupata soko kutokana na athari inayotarajiwa ya kampeni hiyo inayosukuma ununuzi zaidi.

"Wengine wanaonufaika na 'Jibambe Kibabe' ni watumiaji katika kiwango cha baa ambapo kampeni imeandaa ofa nyingi vikiwamo vifaa maalum ili watumiaji wa bidhaa kufurahia na kushiriki na marafiki kwa bei iliyopunguzwa," alitamba.





## Uchumi wa buluu kuinua uchumi wakazi wa Tanga

**Na Oscar Assenga,** TANGA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema kupitia fursa ya uchumi wa buluu wananchi wa Jiji la Tanga, watajiongezea fursa za kiuchumi kupitia miradi ya kilimo cha mwani na jongoo bahari.

Miradi mingine ni unenepeshaji wa kaa, ufugaji wa samaki, kuku na kilimo cha mboga katika Kata ya Tongoni, Masiwani, Tangasisi, Usagara na Central.

Ummy, ambaye ni Mbunge wa Tanga Mjini, aliyasema hayo jana, alipotembelea miradi inayotekelezwa na Taasisi ya Tanga Yetu, kupitia ufadhili wa Shirika la Botnar Foundation.

Katika utekelezaji wa miradi hiyo, fedha zilizotumika hadi sasa ni Sh. bilioni 5.65, ambazo kwa asilimia kubwa zimewasaidia wananchi kujikwamua kiuchumi.

Alisema kutokana na umuhimu wa uchumi wa buluu katika kukuza uchumi wa wananachi, Jiji la Tanga limejipanga kuwa kinara katika miradi hiyo, kwa kutumia fursa ya bahari iliyopo kwenye Ukanda wa Pwani.

Alisema kwa kuwa Mkoa wa Tanga una eneo kubwa la bahari, wamejipanga kuongeza uzalishaji ili kuwa vinara wa kutumia fursa za uchumi wa buluu, kwa maendeleo ya watu.

Alisema kutokana na uwepo wa fursa wanapaswa kulikumbatia zao la mwani kwa sababu ni zao ambalo kilimo chake sio kigumu zaidi na faida yake ni kubwa.

Awali, Mwakilishi wa Botnar Tanzania, Dk. Hassan Mshinda, alimhakikishia Ummy kwamba wataendelea kushirikiana nae na Halmashauri ya Jiji la Tanga katika kutatua kero za maendeleo kwa wakazi wake.

# WWF yazindua mradi wa utunzaji, ulinzi ushoroba

**Na Godfrey Mushi,** LONGIDO

SHIRIKA la Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF) limeutambulisha mradi mpya wa majaribio uitwao 'Wildlife Credit' maarufu kama tuzo, unaolenga zaidi kutoa motisha ya utunzaji na ulinzi wa ushoroba wa Kitendeni.

Ushoroba huo ni mapito ya wanyamapori wanaohama, kati ya Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA) na Amboseli ya nchini Kenya, kutafuta malisho na maji.

Vijiji vinne vya Irkaswa, Kitendeni, Lerang'wa na Kamwanga vilivyoko Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, ambavyo niwanachama waJumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Enduimet (EWMA), ndivyo viilivyoguswa na mradi huo wa miezi 18. Akiutambulisha mradi huo jana kwa wananchi wa vijiji vya Irkaswa na Kamwanga, Msimamizi wa Mradi wa SOKNOT (Southern Kenya, Northern Tanzania), Prof. Noah Sitati, alisema eneo hilo ambalo lina wanachama wengi wa Enduimet WMA, wanataka mradi huo utoe picha na matokeo halisi, kabla ya kutekelezwa katika jumuiya nyingine zote za uhifadhi Tanzania.

"Mnajua kwamba ushoroba wa Kitendeni ni muhimu, kwa kuwa tembo wanatumia na wanyama wengine kutoka kule Amboseli, Kenya mpaka Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro.

"Tumetengeneza huu mradi ili kuvifaidisha vijiji vinne na wakati vikiendelea kutunza ushoroba wa Kitendeni, hiyo inakuwa kama zawadi.

Ni kama tuzo fulani ya kusema hongereni kwa kutunza hii corridor (ushoroba) isikae wazi kwa vile hakuna maendeleo kule ndani.

...Tunatafuta namna ambayo jamii, inaweza kufaidi na ndiyo maana tukatengeneza huu mradi mdogo wa majaribio, ambao unakuja kusaidia jamii iliyojikita kuulinda ushoroba wa Kitendeni."

Kwa mujibu wa Prof. Sitati, moja ya vigezo vitakavyotumika kuonyesha kijiji kimefanikiwa kutunza na kuulinda ushoroba wa kitendeni, ni kuzuia ujenzi wa makazi, shughuli za kilimo, ujangili au uwindaji haramu wa wanyamapori.

"Kuna mambo mengi ambayo yanaweza kuharibu ushoroba kwa mfano kuna majangili wanaweza kuingia na kuua wanyama wakipita, lakini nyie wenyewe ndio macho kwa vile mnajua hiyo ni sehemu yenu.

"Kuna wale watu wanachoma mkaa, ama wanakata miti kama mbao. Wanachukua mali yenu wanapeleka kwingineko. Nasikia upande wa Kenya, majangili wanaua wanyama na hao wanyama ndio wanaoleta utalii katika sehemu yetu ya Enduimet WMA. Tunaita photographic tourism."

Katika mkutano mkuu wa Kijiji cha Irkaswa, wananchi wake wakiwamo Sinati Sangau, Asia Rajab, Joshua Mollel na Sinyoki Melita, kwa nyakati tofauti, walieleza furaha yao namna mradi huo unavyokwenda kuchochea na kuinua maisha yao kiuchumi kutokana na kuwapo kwa ushoroba huo.

Aidha, Silas Mollel, Mkazi wa Kijiji cha Kamwanga alisema, "Unavyokiona Kijiji cha Kamwanga ni mapito ya wanyamapori, wanapita wakishuka kwenda Amboseli, wanapita wakipanda kuja Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro.

...Na saa nyingine wanafanya uharibifu wa mazao yetu kama mahindi na maharage, migomba na mashamba, lakini hatujawaua, tunawatolea ripoti. Leo mmetuletea mradi wenye manufaa kiuchumi, tunaupokea kwa mikono miwili."

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kamwanga, Juma Mohamed, baada ya utambulisho wa mradi huo, aliwaonya wananchi kuacha tabia ya kuua na kula wanyamapori kuanzia sasa, kwa kuwa kigezo hicho kitawanyima fursa ya kunufaika na fedha zitakazotolewa kutokana na mradi wa Wildlife Credit.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Ummy Nderiananga (kulia), akimsikiliza kiongozi wa Konga ya ARIEL Group, Robert William, wakati akikagua baadhi ya bidhaa wanazotengeneza kabla ya kuzungumza na wanachama kutoka konga za watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI mjini Moshi jana. **PICHA MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaombwa kujenga kiwanda kutengeneza vifaa vya utengemao

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WADAU wanaohudumia watoto wenye ulemavu wa akili mkoani Kilimanjaro, wameing'ata sikio serikali, ikiiomba kutafuta wawekezaji watakaojitokeza kujenga kiwanda cha kutengeneza vifaa vya utengemao, kwa ajili ya kusaidia jamii ya watu wenye ulemavu.

Mtawa wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini, Woinde Nkya, ambaye ni Mtaalamu wa Tiba Kazi, anayefanya kazi katika kitengo cha BCC, alisema kwa hali ilivyo sasa ya upatikanaji mdogo wa vifaa vya utengemao, ikiwamo viti mwendo, kuna haja ya kuvutia wawekezaji kujenga kiwanda chake nchini.

Alikuwa akizungumza jana katika Manispaa ya Moshi, wakati wa siku maalumu ya michezo ya watoto wenye ulemavu wa akili, wanaohudumiwa na Shirika la Building Caring Community (BBC) lililoko chini ya Idara ya Udiakonia ya Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT.

"Tunaagiza hivi vifaa nje ya nchi kwa gharama kubwa na kupata bado ni kwa shida. Kama wadau tunaiomba serikali ilitazame hili kwa jicho la tatu.

Idadi kubwa ya wahitaji wanakosa huduma nyingi za utengemao kwa wakati. Tatizo la upatikanaji wa viti mwendo hapa nchini ni changamoto kubwa hasa kwa watoto ambao tayari wameanza kukua na kuhitaji viti hivyo ambavyo husaidia wazazi na walezi kuepuka kuwabeba."


Mratibu wa Huduma za BCC, Mdiakonia Elirehema Kaaya, alisema kwa sasa wanatoa huduma hiyo pekee katika Manispaa ya Moshi lakini kwa mwaka huu huduma hiyo itapanuka kuelekea Wilaya ya Hai na maeneo mengine yanayoguswa na Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT.

"Tuna miaka 16 kwenye huduma hii ya shughuli za utengemao, tukilenga zaidi kuwasaidia watoto na vijana kuanzia umri wa miaka miwili na nusu, kuwafanyisha mazoezi mbalimbali ya utengemao, kufanya tiba inayoendana na therapy na afya," alisema Kaaya.

Aidha, Mratibu wa Afya wa BCC, Godson Mmari, alisema changamoto kubwa wanayokutana nayo kwa sasa ni upatikanaji wa matibabu na uchunguzi wa afya kwa watoto wenye ulemavu wa akili. "Wazazi wengi wenye watoto wenye ulemavu haswa katika Manispaa ya Moshi ni maskini, hawana uwezo wa kulipia matibabu. Tangu kufutwa kwa kadi ya bima ya afya kwa watoto, wameshindwa kabisa kumudu kulipia gharama za matibabu hospitalini.

"BCC tulikuwa tunapata ufadhili wa kulipa Sh. 50,400 kwa kila mtoto lakini sasa hivi kulingana na haya mabadiliko, hiyo bajeti hatuna tena.

Kwa hiyo watoto hawa wanakwama kupata matibabu na ukweli ni kwamba wanatumia dawa kila siku na dawa hizo ni ghali. Kuna dawa inauzwa mpaka Sh. 60,000 kuna nyingine mpaka Sh. 70,000, kwa mzazi inakuwa ngumu."





# Mawakala wa tiketi wadaiwa kuwanyonya wamiliki mabasi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MAWAKALA wanaokatisha tiketi za mabasi katika Stendi ya Mabasi ya Nyamohongolo iliyopo Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza wamedaiwa kuwanyonya wamiliki wa mabasi kutokana na kuwa na asilimia kubwa ya makato hadi kufikia asilimia 40 ya nauli anayolipa abiria.

Hali hiyo imekiibua Chama cha Wamiliki wa Mabasi Nchini (TABOA) mkoani hapa, kulalamikia kero hiyo na kuiomba serikali kuingilia kati kwa kuwaweka mawakala hao chini yao, lengo likiwa ni kuwafanyia tathmini na kuona namna gani wanawaingizia hasara wamiliki hao pamoja na serikali katika upatikanaji mapato.

Kero hiyo imeibuliwa juzi na viongozi wa TABOA Kanda ya Ziwa, Anuar Saidi wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, alipotembelea kituo hicho cha mabasi pamoja na ujenzi wa soko kuu unaoendela jijini Mwanza.

Saidi alisema kuwa katika sekta hiyo udhibiti wa matumizi yasiyo rasmi umekuwa mgumu kutokana na mawakala hao kuwa na jukumu la kuwapangia wamiliki wa mabasi bei na kuwa na udhibiti wa fedha inayotolewa na abiria.

“Katika fedha inayolipwa na abiria, wakala hao wanachukua asilimia 40 ya tiketi moja inayokatwa hali hii siyo ya kawaida,” alisema.

Baada ya kuibuka kwa kero hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, alizitaka halmashauri, viongozi wa TABOA, LATRA pamoja na viongozi wa polisi usalama barabarani kukutana na kuweka taratibu vizuri ili kudhibiti kero za wawekezaji binafsi.

“Lazima watu binafsi tuwatengenezee mazingira mazuri na wenyewe wafurahie kufanya biashara ili wakitoa huduma na wananchi wetu wapate huduma stahiki na hili ndilo kosa tunalolikosea sana,” alisema Makalla.

Aidha, alisema suala la mamlaka kuendelea kushikilia sheria na kanuni limekuwa likisababisha serikali kushindwa kutengeneza mazingira mazuri kwa sekta binafsi kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Katika hatua nyingine Makalla aliagiza makandarasi wanaotekeleza ujenzi wa Soko Kuu la Mkoa wa Mwanza kuharakisha ujenzi wake, lengo likiwa ni kutoa mwanya kwa wafanyabiashara kuendeleza shughuli zao wakiwamo machinga ambao wamekuwa wakikoswa maeneo rafiki ya kufanyia biashara zao.

“Niwahakikishie kuwa soko hili likikamilika wale wote ambao wapo kwenye kumbukumbu watapewa kipaumbele hivyo lazima mhakikishe vifaa vinafika kwa wakati na kazi inafanyika haraka na kwa ufanisi zaidi,” alisisitiza.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano Vivo Energy Tanzania, Grace Kijo (kushoto), akikabidhi funguo ya bodaboda kwa mshindi wa promosheni ya “Jaza Ushinde Tena” na Engen, Hatibu Kusaga, aliyejishindia zawadi hiyo baada ya kushiriki kujaza mafuta kwenye vituo vya Engen, mjini Korogwe, mkoani Tanga mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Migogoro, majungu chanzo viongozi CCM kujiuzulu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KATIBU wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Shinyanga Mjini, Ally Majeshi, amesema chama hicho kinaendelea kupitia hali ngumu kutokana na migongano ya mara kwa mara ya baadhi ya viongozi na wanachama wilayani humo.

Amesema hali imesababisha baaadhi ya viongozi ndani ya chama kujiuzulu. Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa kikao cha sekretarieti ya viongozi wa CCM Wilaya pamoja na kata zote za halmashauri na kueleza kuwa viongozi wengi ndani ya chama wamejiuzulu sababu ya kupewa misukosuko na baadhi ya viongozi wenzao na wanachama.

Viongozi hao ambao hakuwataja majina alisema wameacha nyadhifa zao kutokana na uchonganishi unaoendelea ndani ya chama hicho, hivyo kuwataka kupunguza maneno na kuhakikisha wanafanya kazi katika kufikia na kutatua kero za wananchi.

“Hizo ni tabia za kudhalilishana acheni haiwezekani mtu una majukumu yako lakini unapata muda wa kuanza kutupiana maneno pamoja na kufuatiliana tunahitaji sasa kudumisha amani ndani ya chama na kujenga mshikamano,” alieleza Majeshi.

Naye Katibu wa (UVCCM) Wilaya ya Shinyanga Mjini, Naibu Katalambula, aliwataka viongozi hasa wanawake ndani ya chama hicho kuwa mstari wa mbele kufichiana matatizo yao na siyo kusemana ovyo na kudhalilishana.

Katibu wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake (UWT) Wilaya ya Shinyanga, Sharifa Hassan, aliwataka viongozi wa chama hicho kudumisha umoja, kupendana na kufanya kazi kwa ushirikiano kwani utaratibu wa malumbano hauna tija ndani ya chama hicho.

Hivi karibuni katika kikao cha Baraza la Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) Mkoa wa Shinyanga, kuliibuka tena suala la wajumbe kurekodiana sauti na kwenda kushtakiana kwa wabunge hali ambayo ilidaiwa ni kukigawa chama na kuleta mpasuko.

## Mradi wa maji kunufaisha wakazi 31,423 Sengerema

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

WANANCHI 31,423 kutoka vijiji vya Chifufu, Lukumbi na Nyakahako, Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema wanatarajiwa kuondokona na adha ya upatikanaji wa maji iliyodumu kwa muda mrefu kupitia mradi wa maji wa zaidi ya Sh. bilioni 2.6.

Akitoa taarifa ya mradi huo, mbele ya kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi, Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira (RUWASA) Wilaya ya Sengerema, Mhandisi George Massage, alisema mradi huo utanufaisha wakazi 31,423 kutoka katika vijiji vitatu.

Alieleza kuwa mradi huo utakaodhibiti adha ya upatikanaji wa majisafi na sala katika vijiji hivyo unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 2.68 na kukamilika Septemba 30, mwaka huu.

Aikizungumza baada ya kuweka jiwe la msingi katika mradi huo kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru, Abdallah Shaibu aliwataka wananchi kuhakikisha wanatunza vyanzo vya maji ili kukabiliana na hali ya mabadiliko ya tabia nchi wilayani humo na taifa kwa ujumla.

Alieleza kuwa serikali inatambua shida ambayo kinamama wanakutana nayo katika kutafuta maji safi na salama na ndiyo maana wanafanya juhudi za kuyatatua ili kumtua mama ndoo kichwani.

Katika hatua nyingine Mwenge wa Uhuru ulifungua jengo la dharura katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya Sengerema ambalo litawanufanisha wakazi kutoka kata 26 ndani ya halmashauri hiyo.

Kadhalika Mwenge wa Uhuru uliweka jiwe la msingi katika Shule ya Sekondari Ibondo, kufungua kituo cha mafuta, kupanda miti, kuweka jiwe la msingi kwenye barabara inayojengwa kwa kiwango cha lami yenye urefu wa Mita 970, kufungua vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Msingi Pambalu na kumaliza mbio zake ukielekea katika Wilaya ya Misungwi mkoani humo.



Ukurasa 12

**Jussa anapoiona Zanzibar kama Singapore, asema inawezeka na shida viongozi kutoamua**



Ukurasa 13

Ni mwaka wa pambazuko jipya kisheria Tanzania Bara, Zanzibar




Ukurasa 14

**HALI TETE KENYA RAILA Vs RUTO**
**Rais anapotishia kuwasafirisha pamoja vigogo Kenyatta, Odinga**


# siasa

JUMATANO JULAI 19, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


DANADANA UCHAGUZI TLP

# Msajili Vyama ampasha kaimu wakati wa kuufanya ni sasa

• Wagombea na wajumbe wachekelea, wakubali yaishe

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya viongozi wa Chama cha TLP, kucheza mchezo wa 'paka na panya' hadi kupita miezi minne tangu kuahirisha uchaguzi wa kumpata mwenyekiti wa taifa, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, imeagiza ufanywe mara moja.

Msajili wa Vyama vya Siasa amemwandikia barua, Kaimu Mwenyekiti wa TLP Taifa, Hamad Mkadamu, inayomwagiza aitishe uchaguzi huo haraka iwezekanavyo.

Kwa mujibu wa nakala ya waraka huo, ulioifikia Nipashe hivi karibuni, pamoja na maagizo hayo, barua hiyo iliyosainiwa na Msaidizi wa Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, pia inamtaka Mkadamu aangalie kwanza iwapo chama chao kina fedha za kufanikisha uchaguzi huo.

Itakumbukwa kuwa TLP ilikuwa ifanye uchaguzi huo Machi 6, mwaka huu, lakini ukaahirishwa kutokana na sababu ambazo hata hivyo hazikuwekwa wazi, hali iliyosababisha sintofahamu ndani ya chama hicho.

"Katika barua hiyo ya kumbukumbu: Na. HA 322/362/15/55, Nyahoza anaeleza kuwa kwa mamlaka alionayo, kaimu mwenyekiti, kwa mujibu wa ibara ya 18.3(j) ya katiba ya TLP, anatakiwa kuitisha uchaguzi huo haraka iwezekanavyo."

Anaongeza: "Hivyo, nawashauri wanachama wa TLP kukaa pamoja tena muwe na maelewano, ili kuhakikisha mnaandaa mkutano mkuu na kufanya uchaguzi wa kujaza nafasi ya mwenyekiti wa taifa wa chama chenu," anaelekeza Nyahoza.



Kaimu Mwenyekiti wa TLP Taifa, Hamad Mkadamu.. **PICHA: MTANDAO**

Anafafanua kuwa Machi 22 alipata barua ya malalamiko kutoka kwa Stanley Ndamugoba kuhusu kuahirishwa kwa uchaguzi, kisha Mei akapokea nyaraka nyingine zilizokuwa na malalamiko ya aina hiyo.

Msaidizi huyo wa msajili anasema barua hizo zilitoka kwa Domitana Rwechungura, Abuu Changaa, Felix Sanga, Kinanzaro Mwanga na Aivan Maganza ambao wote walikuwa wagombea wa nafasi hiyo.

**KATIBA YA TLP**

Akichambua katiba ya chama hicho, Nyahoza anasema ibara ya 19.9 inaeleza kuwa kipindi cha uongozi ndani ya chama ni miaka mitano, na kwamba TLP ilifanya uchaguzi mwaka 2020, na kufafanua kuwa tangu wakati huo, miaka mitano ya kufanya uchaguzi mwingine haijamalizika.

Lakini anakariri ibara ya 24 ya katiba ya chama hicho kuwa nafasi ya uongozi ikiwa wazi kwa sababu yoyote ile, sekretarieti itaandaa utaratibu wa kujaza nafasi hiyo mara moja na kwamba pengo hilo lisifanye shughuli za chama zisiendelee hadi pale tu katiba hiyo itakapokataza.

"Nimesema katiba na kanuni za TLP, sijaona sehemu iliyoweka ukomo wa kiongozi kukaimu, yaani muda wa kujaza nafasi ya uongozi iliyo wazi. Hata hivyo, ibara ya 24 inaeleza kuwa nafasi ya uongozi ikiwa wazi inapaswa kujazwa mara," anasema.

Anaongeza kuwa kwa kuwa aliyekuwa mwenyekiti wa chama hicho, Augustine Mrema alifariki Agosti 21 mwaka 2022, chama kikajaribu kufanya uchaguzi Machi 6 mwaka huu, lakini haukufanyika, na kwamba chama kinatakiwa kuandaa uchaguzi mwingine.

Msajili msaidizi huyo anasema hatua ya viongozi wa chama hicho kufanya uchaguzi kuziba nafasi ya uongozi uliyo wazi, watakuwa wametimiza dhana ya mara moja inayoelekezwa katika katiba ya TLP.

"Kaimu Mwenyekiti wa TLP taifa, anapaswa kuitisha mkutano wa mkuu mapema iwezekanavyo, ingawa ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inatambua kuwa kuandaa mkutano mkuu wa chama kunahitaji fedha za kuwezesha shughuli hiyo ifanyike na maandalizi ya kiutawala," anasema.

Hata hivyo, anawataka wanachama wa TLP kuelewa kuwa wakati mwingine sio rahisi kuandaa mkutano mkuu siku chache baada ya nafasi ya uongozi kuwa wazi kutokana na ugumu wa kupata fedha.

**UCHAGUZI WANUKIA**

Kaimu Mwenyekiti wa TLP, Hamad Mkadamu, anakiri kupokea maagizo kutoka Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na kufafanua kuwa anajiandaa kukutana na viongozi wenzake kupanga tarehe ya uchaguzi.

"Kwa sasa niko Mkutano wa Jukwaa la Demokrasia Afrika huku jijini Arusha, nikirudi nitafanya kama ambavyo msajili ameelekeza, hivyo kila kitu kitajulikana tukishakutana," anasema Mkadamu.

Wakati akisema hayo, mmoja wa wagombea hao, Ivan Maganza, anasema suala la ukosefu wa fedha za kuendesha uchaguzi si tatizo, kwa maelezo kuwa watazipata kwa wapenzi wa chama hicho.

"Ninafurahi kwani malalamiko yetu yamefanyiwa kazi, hivyo tunaomba maagizo ya msajili yatekelezwe, pesa za uchaguzi zitapatikana, lakini wajumbe wako tayari kujigharamia kila kitu," anasema Mhandisi Maganza.

Mmoja wa wajumbe wa mkutano mkuu ambaye ni Mwenyekiti wa TLP Mkoa wa Tabora, Mussa Amir anasema yuko tayari kujigharamia kila kitu hata kama uchaguzi huo ukifanyika leo.

"Mwaka kesho tuna uchaguzi wa serikali za mitaa, tutashirikije katika uchaguzi huo bila kuwa na mwenyekiti wa chama taifa? Wajumbe wengi tuko tayari kujigharimia ili tupate mwenyekiti mpya," anasema Amir.

Aidha, anamwomba kaimu mwenyekiti kutekeleza maagizo ya msajili wa vyama bila kusita kwa lolote, kwa maelezo kuwa tangu uchaguzi ulipoahirishwa, wajumbe walichukia kuona mmoja wa viongozi wa juu akiuvuruga, na kwamba watahakikisha hachaguliwi.

# Jussa anapoiona Zanzibar kama Singapore, asema inawezekana shida viongozi kutoamua

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

ZANZIBAR ina sifa za kufikia maendeleo ya Singapore kwa muda mfupi, taifa ambalo Waziri Mkuu Lee Kuan, anaendelea kukumbukwa mpaka leo kwa kuwaletea mageuzi ya kasi kiuchumi yaliyofanikisha maendeleo makubwa kijamii, iwapo viongozi wataamua.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya ACT-Wazalendo, Ismail Jussa Ladhu, anasema na kuwanyooshea kidole viongozi wanaotumia rasilimali za umma kwa maslahi binafsi akisema wanachelewesha maendeleo.

Mataifa ya Singapore, Hong Kong, Korea Kusini na Taiwan magwiji wa uchumi au 'Asian tiger economies' yamekuwa na ukuaji wa kasi ya juu wa uchumi. Mwanzoni yalitegemea kilimo duni miaka ya 1960, lakini kuanzia miaka ya 1990 yakabadilika na kuwa nchi zilizoendelea kiviwanda na kiteknolojia.

Akizungumza katika kongamano la vijana wa chama hicho lililofanyika visiwani Zanzibar mwanzoni mwa mwezi huu, Jussa anasema Wazanzibari wanataka mageuzi makubwa katika nchi na rais atakayeyaleta akumbukwe daima.

Anasema kiongozi huyo atakumbukwa na kuheshimika kwa kuunda taasisi imara za mageuzi ya kiuchumi, kijamii na kuibadili nchi kimaendeleo.

Katika kongamano hilo la vijana wa ACT-Wazalendo, imezindua kampeni ya 'Zanzibar na Mimi, Mimi na Zanzibar' katika kuelekea mchakato wa katiba mpya kabla ya uchaguzi mkuu wa 2025.

Jussa anawataka vijana wairejeshe Zanzibar inarejea mahala pake, katika kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 ikiwamo kuheshimiwa misingi ya demokrasia na haki za binadamu.

Anasema imani yake ni kwamba ACT -Wazalendo, uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 itaongoza nchi na kuweka historia ya kuwa na rais atakayeheshimu katiba na sheria.



Kongamano la Vijana wa ACT- Wazalendo. **PICHA: ACT-WAZALENDO**

### AMPONGEZA RAIS SAMIA

Akizungumzia uhuru wa kujieleza, mshauri wa ACT-Wazalendo, Masour Yussuf Himid, anasema tangu uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, hali imebadilika na amefungua milango ya demokrasia baada ya vyama vya siasa na wananchi kupata uhuru wa kutoa maoni yao.

"Mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni Rais Samia amefanya kazi kubwa ya kuifungua milango ya demokrasia nchini baada ya kufungwa kwa muda wa miaka saba na mtangulizi wake," anakumbusha Mansour.

Anadai nchi ilipitia katika kipindi kigumu na taarifa za utekaji watu, mauaji, kushambuliwa, maiti kuokotwa kwenye viroba, ukandamizaji wa haki na kufutwa kwa haki za vyama vya siasa ni miongoni mwa yaliyoshuhudiwa.

Aidha, anasema hivi sasa kuna ahuweni baada ya kuja Rais Samia na kukumbusha kuwa hakuna utekeaji, wala watu kuokotwa miili iliyoharibika katika viroba na kwamba Watanzania wanafanya shughuli za kisiasa bila kukwamishwa . Tena wanayo haki ya kusema ya moyoni na pia kukusanyika na mikutano inaendelea hata kama wanatofautiana na CCM.

"Lakini suala la kujiuliza je, hilo linatosha? Tutaendelea kusubiri bahati nasibu kwamba leo aje rais mwema au tunahitaji taasisi na vyombo madhubiti kuhakikisha watu 'waovu' hawapati nafasi ndani ya nchi yetu?"Anadai Mansour.

Aidha, anawataka vijana wa chama hicho kusimama imara ili kukiondoa chama tawala madarakani katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Anawaambia kimsingi chama hicho kimeshamalizika Zanzibar, na kutoa mfano uchaguzi uliofutwa mwaka 2015 akisema njia pekee ya kuiwezesha Zanzibar kupiga hatua kimaendeleo ni nchi kuwa na katiba mpya itakayoakisi matumaini yao, akiwahimiza kusimama imara kwa pamoja kutetea maslahi ya Zanzibar.

### OTHUMAN ATAJA GAZA

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud, anadai Zanzibar hugeuka kama Ukanda wa Gaza na watu kujeruhiwa na wingine kupoteza maisha wakati wa uchaguzi kutokana na kutoheshimiwa misingi ya demokrasia na haki za binadamu.

Anasema Zanzibar inahitaji mifumo ya sheria kuimarishwa ikiwamo kuwa na mahakama huru inayotekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa hatua itakayojenga imani kwa wawekezaji wakubwa kwa wadogo.

"Lakini suala la kujiuliza je, hilo linatosha? Tutaendelea kusubiri bahati nasibu kwamba leo aje rais mwema au tunahitaji taasisi na vyombo madhubuti kuhakikisha watu 'waovu' hawapati nafasi ndani ya nchi yetu?"Anadai Mansour.

Hata hivyo, anasema ili ipige hatua ya maendeleo lazima iwe na mamlaka kamili ya kusimamia rasilimali zake za kiuchumi na vyanzo vya mapato ikiwamo mamlaka ya kodi.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais anadai kukosekana kwa mamlaka kamili kunaikwamisha kuchimba mafuta na gesi kwa vile haiwezi kuchimba rasilimali hiyo bila ya kuwa na mipaka ya bahari.

Anataja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa inaeleza kuwa suala la mipaka ya nchi linasimamiwa na Serikali ya Muungano, ndiyo maana utafiti wa uchimbaji wa mafuta umekwama kwa zaidi ya miaka saba.

Anasema kwamba sekta ya usafirishaji wa anga, gesi asilia na mafuta ni miongoni mwa fursa muhimu za kiuchumi zilizopo zinazoweza kupunguza tatizo la vijana kukosa ajira na kuwainua kiuchumi.

Othman anasema Zanzibar inao uwezo mkubwa wa kupiga hatua kiuchumi kupitia sekta hizo pekee na nyingine kadhaa na hilo litafanikishwa kwa kuwapo mipango na usimamizi bora pamoja na uwezo wa kupanga na kuamua wenyewe kama ilivyofanyika katika nchi nyingine dunaini.

Anaamini kuwa hatua hiyo inaweza kushawishi kampuni za fedha na uwakezaji kuanzisha miradi mikubwa ya kibiashara kwa imani kwamba wataweza kupata faida kupitia shughuli wanazoanzisha na pia kusaidia ajira kwa wananchi kwa vile kutakuwapo masharti bora yanayosisitiza kutoa kipaumbele kwa wazalendo.

Aidha, anasema uchumi wa Zanzibar hivi sasa umepitwa na nchi ndogo kama vile Maritius na nyingine zenye asili ya visiwa ambazo Zanzibar ilikuwa mbele zaidi kiuchumi wakati wa mapinduzi ya uhuru mwaka 1964.

Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Othman anasema suala la kuondoa umaskini linawezekana kwa sababu ipo mifano ya nchi nyingi za visiwa vidogo ambavyo havina historia ya utukufu na nafasi kama ya Zanzibar.

Anasema njia pekee iliyosaidia nchi hizo ni kuwapo mamlaka za usimamizi na za kupanga mipango bora wenyewe na kuweza kuzitumia vyema fursa za kiuchumi walizonazo na hivyo kujiimarisha kiuchumi na kupiga hatua kimaendeleo.

Anasema nchi zenye kufanana na Zanzibar ni vigumu kujikwamua kiuchumi iwapo hazitakuwa na mamlaka na uwezo wake wa kujipangia kodi jambo analodai linaweza kuwavuta wawekezaji wakubwa kutoka nje kuwekeza na kuondoa matatizo likiwa la ajira kwa vijana na kupunguza umaskini.

"Huwezi kuendesha nchi katika mtindo unaoendelea sasa huku ukiwa huna mamlaka na uwezo wa kufanya maamuzi katika masuala mbalimbali na ukaweza kupiga hatua na kwamba suala kuwepo Zanzibar yenye umoja ni miongoni mwa nyenzo muhimu za kuleta maendeleo kwa haraka," anasema.

Anawataka vijana wa Zanzibar kuungana na kuwa kitu kimoja katika kupambania Zanzibar yenye maendeleo, kujenga umoja na hivyo kuondoa tatizo la umaskini ambalo linawezekana bila miujiza kwa kuwa na uongozi wa kizalendo na unaoungwa mkono na wananchi.

# Ni mwaka wa pambazuko jipya kisheria Tanzania Bara, Zanzibar

**Na Restuta James**



Kutoka kushoto; Katibu wa LRCT, Grrifin Mwakapeje, Mwenyekiti wake, Jaji January Msoffe, Mwenyekiti wa LRCZ, Hadija Shamte Mzee na Katibu Musa Kombo Bakari. **(PICHA: RESTUTA JAMES)**

MFUMO thabiti wa kisasa na wa kisheria ndiyo msingi wa jamii yenye haki na ustawi, unaowezesha kuwa na mazingira wezesheji ya ukuaji wa uchumi, uwekezaji pamoja na mshikamano wa Tanzania.

Jaji Mstaafu, January Msoffe, anasema hayo anapozungumza wakati wa kusaini hati ya makubaliano ya ushirikiano kati ya Tume za Kurekebisha Sheria za Tanzania (LRCT) na Zanzibar (LRCZ) jijini Dar es Salaam na kuashiria enzi mpya ya Tanzania yenye sheria zinazolinda haki na kuimarisha ustawi wa pande mbili za Muungano.

Anaueleza ushirikiano huo kuwa utakuwa jukwaa muhimu la kubadilishana ujuzi, utaalamu na mbinu bora katika nyanja ya mageuzi ya sheria kwa taifa na kwamba kwa pamoja watatumia nguvu zao ili kuimarisha utafiti wa kisheria, mapitio na tathmini ya sheria zilizopo.

Anawaambia wajumbe kuwa aidha, utaongeza ushirikiano, kuzisaidia tume kushughulikia haraka masuala muhimu yanayohitaji juhudi za pamoja na kupata ufumbuzi kwa manufaa ya pande zote.

"Napenda kuahidi kuwa tutaunganisha rasilimali, vipaji na uzoefu ili kushughulikia changamoto zinazojitokeza za kisheria kama vile usalama wa mtandao, ulinzi wa mazingira, haki za binadamu na maendeleo ya kiuchumi," anasema Jaji Msoffe.

Anaongeza: "Tume ya hizo zina maono yanayofanana ya kuhakikisha kwamba mifumo yetu ya sheria inaendana na mabadiliko yanayotokea katika jamii kukidhi mahitaji yanayoendelea ya kijamii na kwa kuzingatia mila, tamaduni na desturi zetu kwa maendeleo endelevu."

Kadhalika, anasema, zimeingia makubaliano ya ushirikiano ambayo yataziwezesha kuunganisha rasilimali walizonazo kutekeleza majukumu yake kama kufanya utafiti, kupitia na kutathmini sheria.

Mwenyekiti wa LRCT, Jaji Msoffe anaeleza kuwa tume hizo zinatekeleza majukumu yanayofanana na wamekuwa wakishirikiana kwa muda mrefu, hivyo kuunganisha nguvu kwa kuwa na mkakati wa kimaandishi ni hatua muafaka wa kufungamanisha mahusiano yao.

Aidha, ushirikiano huo unalenga kuunganisha juhudi za tume hizo katika kuimarisha mfumo wa kisheria na kuendeleza utawala wa sheria katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Anasema tume hizo zina majukumu makubwa matatu ambayo ni kufanya utafiti wa kisheria, kuzipitia na kutathmini sheria mara kwa mara ili kushughulikia changamoto zinazojitokeza na kulinda haki za msingi kwa maendeleo ya jamii.

Jaji Msoffe anasema makubaliano hayo yanaimarisha msingi wa mfumo wa kisheria unaozingatia utawala bora na wa sheria.

Mwenyekiti wa LRCZ, Hadija Shamte Mzee, anasema ushirikiano huo utapunguza gharama za utafiti wa kisheria kwani nyingi zitafanywa kwa pamoja na kuleta matokeo yanayohitajika kwa pande zote.

"Tukiongeza nguvu pamoja ni tofauti na kila mtu angefanya kitu kwa upande wake, tofauti na kila mmoja akisema anakaa kama yupo kwenye kisiwa na kufanya kwa utaratibu wake mwenyewe," anasema.

Nia ya tume hizo ni kuzijengea jamii uelewa wa sheria na kutimiza malengo ya serikali na kupunguza gharama kwenye tafiti za kisheria, anasema.

LRCT na LRCZ, zitatumia rasilimali walizonazo kufikia malengo yanayokusudiwa ndani ya muda mfupi, mwenyekiti huyo, anasema na kuongeza kuwa wapo wadau wa maendeleo wenye rasilimali zinazoweza kusaidia kazi za tume hizo, hivyo ni wajibu wao kutumia nafasi hiyo kusaidia umma.

"Tunatarajia kasi iongezeke na kile kinachofanywa na tume zetu kionekane na naamini serikali itatumia zaidi tafiti zetu," anasema.

Maneno ya Mwenyekiti huyo wa LRCZ, yanaakisi lengo kuu la tume hiyo ambalo ni kujenga uwelewa wa sheria kwa jamii ili iweze kufahamu haki zao za kisheria na kushiriki katika utafiti wa mapitio ya sheria.

Aidha, dhamira ya tume hiyo visiwani Zanzibar ni kuzirekebisha ili zilingane na mwelekeo wa mabadiliko na mahitaji ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kwa wananchi.

Anaongeza kuwa dira ya LRCZ ni kuwa na sheria zinazokidhi haja kwa maendeleo ya watu wa Zanzibar na kwa upande wa LRCT, ni kuwa taasisi inayoaminiwa kwenye maboresho ya sheria ili kufikia utawala wa sheria kwa maendeleo ya jamii, wakati dhima yake ni kufanya mapitio na utafiti wa kuboresha sheria za Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania kulingana na misingi ya Katiba kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

### MKAKATI LRCT

Makubaliano ya ushirikiano wa tume hizo yamesainiwa wakati ambao LRCT inatekeleza mpango mkakati wa tatu tangu kuanzishwa kwake mwaka 1983. Mpango huo ni wa mwaka 2022/2023-2025/2027.

Pamoja na mambo mengine, mkakati huo unatoa mwelekeo kutimiza lengo la kuwa na mfumo wa kisheria wezeshi kwa maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Mpango huo unazingatia mpango mkakati uliopita wa 2018/2019 - 2020/2021, Dira ya Taifa ya 2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Awamu ya Tatu 2020/21 - 2025/26, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Dira ya Afrika 2063 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025.

Katika mpango mkakati wa 2018/19 - 2020/21, LRCT ilifanikiwa kuwasilisha ripoti saba zilizopendekeza maboresho ya sheria mbalimbali nchini.

Mpango wa sasa ambao upo kwenye tovuti ya tume hiyo, umejikita kwenye malengo manne ya kimkakati ambayo ni; kupunguza maambukizi ya VVU/UKIMWI na kuboresha huduma za usaidizi, kuimarisha utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa kupambana na rushwa, uwezo wa kitaasisi katika kutoa huduma na kurekebisha na kuandaa sheria. Tume inalenga kuboresha mifumo, taratibu, mageuzi na uandaaji wa sheria.

Katibu Mtendaji wa LRCZ, Musa Kombo Bakari, anasema makubaliano hayo ni ya miaka mitano na kwamba yataundiwa timu itakayokutana mara mbili kwa mwaka ili kusimamia utekelezaji wake.

Katibu Mtendaji wa LRCT, Griffin Mwakapeje, anasema tume zimeunganisha nguvu kutokana na kuwa zinafanyakazi zinazofanana hivyo ushirikiano utaongeza tija kwa kutumia rasilimali zilizopo.

### MIRADI INAYOENDELEA

Makubaliano hayo yamekuja wakati ambao tume inapitia mfumo wa utoaji haki katika mahakama za mwanzo, ambayo yanalenga kubainisha endapo sheria za mwenendo wa mashauri zinazotumika Mahakama za Wilaya, za Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu zinaweza kutumika katika Mahakama za Mwanzo, ili kuboresha mfumo wa utoaji haki.

Kazi nyingine ni tathmini ya mfumo wa sheria zinazosimamia usafiri kwa njia ya maji na ule wa ardhini, ili kubainisha mafanikio na changamoto zinazokabili utekelezaji wa sheria zinazosimamia sekta hiyo ili kutoa mapendekezo yatakayosaidia kuboresha utekelezaji.

Jingine ni mapitio ya mfumo wa sheria zinazosimamia uchaguzi na vyama vya siasa Tanzania, yanayolenga kubainisha changamoto za kisheria na kitaasisi ambazo zinaukabili uchaguzi.

Aidha, LRCT iko katika hatua za awali za maandalizi ya mpango wa mapitio ya sheria mbalimbali wa mwaka 2023-2025, ili kuhakikisha Tanzania inakuwa na sheria zinazoendana na wakati kwa maendeleo endelevu.

JUKWAA LA VIONGOZI

HALI TETE KENYA RAILA VS RUTO

# Rais anapotishia kuwasafirisha pamoja vigogo Kenyatta, Odinga

• Raila apashwa 'acha umesumbua miaka 40', atishwa 'atakufa' J'tano na kuzikwa J'mosi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI viongozi wa serikali na wa upinzani wakitunishiana misuli kuzidisha uhasama kuhusu maandamano ya kulalamikia Sheria ya Fedha ya 2023, upinzani unazidi kuitesa serikali ukisema leo ni leo yatafanyika maandamano nchi nzima.

Aidha, serikali nayo inaahidi kuanza siku kwa kuwashughulikia vinara wa upinzani, wanaodaiwa kuyadhamini ikisema wana lengo la kuharibu mali.

Rais William Ruto, Naibu Rais Rigathi Gachagua, Waziri wa Usalama wa Ndani, Kithure Kindiki, Waziri wa Biashara na Viwanda Moses Kuria, na viongozi wengi wa Bunge la Kitaifa na Seneti ni miongoni mwa wanaotishia kupambana na Azimio na Rais Mstaafu Uhuru Kenyatta wanayedai, anafadhili maandamano hayo.

Akihutubia wiki iliyopita huko Nakuru, Rais Ruto anatishia hatawakubali Raila Odinga na Uhuru Kenyatta kuiharibu nchi kwa kisingizio cha maandamano, akiahidi 'atawasafirisha' pamoja.

"Azimio itafanya maandamano mara tatu kuanzia wiki hii Jumatano, Alhamisi na Ijumaa. Ninataka nikuhakikishie kuwa njia hiyo uliyochukua niko nawe ana kwa ana". Odinga anamtambia Ruto.

Rais Ruto anamjibu: "Haiwezekani. Maandamano hayawezi kufanyika tena Kenya. Hiyo siku ya Jumatano wanayosema hilo halitawezekana.

Anawachimbia mkwala huo anapohutubia huko Nakuru na kuungwa mkono na Naibu Gachagua, anayeeleza kushangaa kuhusu lengo kuu la Odinga kwenye maandamano.

"Lengo ni nini baada ya kukataliwa na Wakenya mara tano?" Anahoji na kuongeza Raila, una miaka 80. Wakenya walikukataa mara tano ulipowania urais. Unataka nini?

"Ninasema kwa niaba ya serikali, yametosha. Raila Odinga hatakubalika tena chini ya mpango wowote ule kuzua ghasia, kusababisha maafa na kuharibu mali. Hayatafanyika tena. Mtu mmoja hawezi kuwasumbua Wakenya kwa miaka 40."

Waziri wa Usalama wa Ndani, Profesa Kindiki Kithure, akamwonya Odinga na wafuasi wake kuwa watajutia vitendo vyao Jumatano, Alhamisi na Ijumaa.

"Mtajutia yale mnayopanga. Tutakabiliana nanyi vilivyo. Hatutakubali maafa au uharibifu zaidi wa mali. Vikosi vyetu vya usalama vitakuwa tayari kumkabili yeyote anayedhani atatumia maandamano kuvuruga maisha ya Wakenya wengine."

Waziri wa Biashara na Viwanda, Moses Kuria, akawaka: "Nina imani kubwa kuwa uharibifu wa kiuchumi unaoendeshwa na upinzani hautahujumu ajenda yetu ya maendeleo."

Kwenye mtandao wa Twitter, waziri huyo anaandika bila kutaja aliyemrejelea, "Atakufa Jumatano tarehe 19 na azikwe Jumamosi tarehe 29. Jowi!"





Raila Odinga . **PICHA: MTANDAO**

> "Tumekusanya ushahidi wa kutosha kuthibitisha makabiliano kati ya Azimio na Kenya Kwanza sasa yamegeuka kuwa uhalifu dhidi ya binadamu," anasema Profesa Ogolla.

Aidha, kwenye taarifa ya pamoja, baada ya mkutano wa wabunge wa Kenya Kwanza uliofanyika katika Ikulu ya Nairobi, Ijumaa, unatoka ujumbe unaosema "Ujumbe wetu ni mmoja kwa Odinga; Jumatano tutasimama kidete kuilinda nchi, mali, demokrasia yetu na watu wetu."

Hata hivyo, Odinga amesisitiza kuwa hatatishwa ili alegeze msimamo na kuacha kupinga Sheria ya Fedha 2023 huku akidai serikali imebuni kikosi cha "kuwamaliza" viongozi wa Azimio na waandamanaji.

Odinga anajibu: "Wakenya hawajawahi kushindwa katika mapambano ya ukombozi. Tunapigwa, kukamatwa na kuuawa lakini hatushindwi. Tumewahi kuzuiliwa bila kushtakiwa na kuwa waathiriwa wa ukatili wa polisi na hata mahakama iliyotii serikali na bado hatukushindwa."

Anasisitiza kuwa maandamano ya siku tatu kuanzia leo yatafanyika licha ya viongozi wa serikali kutishia kuwachukulia hatua kali ikiwamo "kuwasafirisha" vinara wa upinzani, Rais Ruto anasema.

**KAKA WA RAILA AJIBU**

Viongozi wa Azimio wanatisha kuwa nchi itavurugika zaidi iwapo serikali itawakamata au kuwadhuru vinara wao. Seneta wa Siaya Oburu Odinga, kaka wa Raila, anasema hatua kama hiyo itagawanya nchi.

"Tuna habari unataka kumuua kaka yangu. Tunaonya wanaohusika na njama hizo sasa wasijaribu uhalifu huo kwa kuwa hali inaweza kuwa mbaya zaidi."

Kiongozi wa wachache katika Bunge la Kitaifa Opiyo Wandayi, anasema nchi itasambaratika serikali ikimkamata au kumdhuru Odinga. Kiongozi wa NARC Kenya Martha Karua ambaye ni kinara mwenza wa Azimio anasema wanaota maandamano ya kulalamikia gharama ya juu ya maisha hayatafanyika wanaota mchana.

**RUTO ICC TENA**

Vuguvugu la Operation Linda Ugatuzi limewasilisha ombi Mahakama ya Kimaitaifa ya Uhalifu (ICC) ikitaka kuchunguza uharibifu wa mali na maafa wakati wa maandamano ya Jumatano wiki iliyopita.

Kwenye taarifa aliyoisoma kwa wanahabari jijini Nairobi mnamo Jumatatu, Julai 17, 2023.

Kiongozi wa vuguvugu hilo Fred Ogolla, anawaambia wanahabari jijini Nairobi kuwa polisi wamewaua kwa makusudi waandamanaji.

"Tumekusanya ushahidi wa kutosha kuthibitisha makabiliano kati ya Azimio na Kenya Kwanza sasa yamegeuka kuwa uhalifu dhidi ya binadamu," anasema Profesa Ogolla.

"Kwa hivyo, tumeiandikia barua ICC ili ichukue hatua kwa sababu moja kati ya wajibu wake ni kuzui uhalifu dhidi ya binadamu."

Profesa Ogolla, anasema mahakama hiyo yenye makao yake jijini The Hague, Uholanzi, lazima iwachunguze wanasiasa wa Kenya Kwanza ambao anadai wanafadhili na kuhimiza mauaji ya waandamanaji wanaolalamikia kupanda kwa gharama ya maisha.

Wanataka ICC kuwachukulia hatua Waziri wa Usalama Profesa Kithure Kindiki, Inspekta Jenerali wa Polisi Japhet Koome na maofisa wakuu wa serikali ambao wamekuwa wakitoa vitisho dhidi ya maisha ya vinara wa Azimio.

"Tumeandaa mkutano na maofisa wa ICC kwa njia ya mtandao ambao tutawasilisha malalamiko yetu kwao pamoja na ushahidi ambao tumekusanya kutoka kaunti zote," anasema Profesa Ogolla, ambaye ni mwasheria.

Operation Linda Ugatuzi pia iliwakashifu wabunge wa Kenya Kwanza ambao walikutana na Rais William Ruto katika Ikulu ya Nairobi Jumamosi asubuhi kupanga mikakati ya kukabiliana na waandamanaji wa Azimio.

"Ni makosa kwa wabunge kuagizwa kukusanya magenge yao ya wahalifu kukabiliana na waandamanaji Jumatano. Hatua kama hii inaweza kusababisha machafuko makubwa na vifo vya watu wengi zaidi nchini," anaongeza.

Anatoa wito kwa Rais Ruto kufanya mazungumzo "ya haki" na kiongozi wa Azimio Raila Odinga ili kuzuia ghasia kulipuka nchini Jumatano.

Hatua ya vuguvugu hilo kuitaka ICC kuingilia kati maandamano ya Azimio imejiri siku moja baada ya kiongozi wa chama cha Wiper Kalonzo Musyoka kudokeza kuwa upinzani utawasilisha kesi katika mahakama hiyo

Akiongea baada ya kuhudhuria ibada ya Jumapili Musyoka anasema Azimio itawasilisha kesi dhidi ya Inspekta Jenerali Koome.

Ni kufuatia kile alichodai ni hatua ya maofisa wa polisi kuwaua kwa risasi waandamanaji Jumatano jijini Nairobi, Mlolongo, Kitengela, Emali na Kisumu.

**MITANDAO**





# TFRA kusambaza mbolea, kuimarisha ukaguzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti na Ununuzi wa Mbolea Tanzania (TFRA), imesema kwa mwaka wa fedha 2023/24 mbolea tani 850,000 itasambazwa kwa kuanza na kanda tano ili kuimarisha ukaguzi wa mbolea, mbegu na viuatilifu.

Akizungumza jana jijini hapa, Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dk. Stephan Ngailo, alitaja kanda hizo ni ya Kati, Nyanda za Juu Kusini, Kaskazini, Kanda ya Ziwa na Mashariki ili wakulima wapate mbolea bora.

Dk.Ngailo alisema kwa mwaka huo mamlaka itaratibu upatikanaji na usambazaji wa mbolea nchini tani 850,000, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa utoaji wa mbolea ya ruzuku, kuendelea kudhibiti ubora wa mbolea, kuhamasisha uwekezaji katika ujenzi wa viwanda vya kuzalisha mbolea nchini, kushirikiana na wadau kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea na uimarishaji wa maabara ya uchambuzi wa mbolea.

Kuhusu ukaguzi, alisema idadi ya wafanyabiashara wanaokaguliwa imeongezeka kila mwaka kutoka 1,000 (2020/21) hadi 3081 (2022/23) sawa na asilimia 84 ya lengo la kukagua wafanyabiashara 3,649.

Aidha, alisema katika ujenzi wa maabara ya kitaifa ya kudhibiti ubora wa mbolea umekamilika na shughuli za uchambuzi wa mbolea zimeanza mwezi huu.

Hata hivyo, alisema utashi wa kisiasa uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika kukuza na kuendeleza tasnia ya mbolea nchini hadi kufikia Juni 30,2023 upatikanaji wa mbolea ulifikia tani 1,115,841 sawa na asilimia 139.48 na kuvuka lengo kabla ya miaka miwili ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020/25).

“Katika Ilani ya uchaguzi ya CCM (2020-2025) inaeleza na kuelekeza kuwa itaongeza usambaji wa mbolea ya pembejeo za kilimo kwa gharama nafuu ikiwa ni pamoja na mbolea, kuongeza upatikanaji wa mbolea kutoka tani 586,604 mwaka 2019/2020 hadi tani 800,000 mwaka 2020/25,” alisema.

Alisema pia kuhamasisha ujenzi wa viwanda vipya vya mbolea na uwekezaji katika viwanda vya kuzalisha mbolea, chokaa kwa ajili ya kilimo na viuatilifu ifikapo 2025 hadi sasa viwanda vya mbolea 17 vinazalisha mbolea kati ya hivyo viwili ni vikubwa na 15 vya kati na vidogo.

Pia, kuimarika kwa mifumo ya upatikanaji na biashara ya mbolea nchini kutoka tani 543,043 (2018/19) hadi tani 1,115,841 (2023/24), kuongezeka kwa wafanyabiashara wa mbolea nchini kutoka 51 (2012/13) hadi 4,562 (2022/23).

Vilevile, kuongezeka kwa viwanda vinne (2016/2017) hadi 17 (2022/23) na kati ya hivyo kiwanda kikubwa kimoja cha Itracom kimeanza uzalishaji rasmi mwaka 2022/23.

“Kiwanda hiki kimeenda kuchangia ongezeko la uzalishaji wa ndani kutoka tani 28,318 (2018/19) hadi kufikia 164,792 (2022/23) sawa na asilimia 25 ya mahitaji,” alisema.

## Madiwani, watendaji watakiwa kudumisha ushirikiano

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewataka madiwani na watendaji wa halmashauri kudumisha ushirikiano na kujiepusha na vitendo vinavyosababisha kutopata hatisafi.

Rai hiyo aliitoa jana kwenye Baraza la Maalum la Madiwani kupitia na kujadili hoja za halmashauri zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) uliofanyika jijini hapa.

“Umoja na ushirikiano wenu mkubwa mlionao umesababisha mafanikio haya makubwa yanatokana na uwepo wa ushirikiano chanya baina yenu waheshimiwa madiwani, watendaji wa halmashauri, viongozi na wadau mbalimbali,” alisema.

Aliwataka kudumisha ushirikiano huo ili halmashauri kuendelea kupata hati safi katika kaguzi zote kila mwaka.

“Hongera sana hati hii safi ya ukaguzi inalifanya Jiji la Dodoma kuendelea kupata kwa miaka minne mfululizo kuanzia mwaka 2017/2018 na kitendo hiki kimelipa heshima Jiji la Dodoma na Mkoa wa Dodoma na taifa kwa ujumla kwa kweli mmetupa heshima wote,” alisema.

Aliwahimiza kuhakikisha wanajibu hoja zote za ukaguzi za CAG ili zifungwe kwa kuzingatia sheria na taratibu za serikali.

Naye Meya wa jiji hilo, Prof. Davis Mwamfupe, alisema kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza taasisi kufuata maagizo na kanuni kwenye matumizi ya fedha za serikali.

Awali, akiwasilisha taarifa ya CAG, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Francis Kaunda, alisema halmashauri ilikuwa na hoja 54 kati hizo 21 zilikuwa za miaka ya nyuma na 33 zilikuwa za mwaka wa fedha 2021/2022.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (wa pili kushoto), akiwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Gerald Mweli (kushoto), wakipokea mavuno ya kwanza ya bidhaa za bustani kutoka kwa vijana wa Mradi wa Jenga Kesho yako Bora (BBT) wa kituo cha Bihawana mkoani Dodoma jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

## Mzee afariki dunia kwa kung’atwa na nyuki sherehe kuwatoa watoto suna

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKAZI wa Kikuyu jijini Dodoma, Abinel Chikataa (71), amefariki dunia kwa kung’atwa na nyuki kwenye sherehe za kuwatoa watoto suna.

Nyuki hao waliokuwa jirani na makazi ya watu walisababisha madhara hayo baada ya watoto kuchokozwa na watoto waliokuwa wakicheza kwenye eneo hilo.

Kutokana na kifo hicho, wananchi wameshauriwa kutoa taarifa kwa maofisa nyuki na watendaji wa serikali wanapoona kuna nyuki wapo kwenye makazi hayo ili kudhibitiwa kabla ya kuleta madhara.

Diwani wa Kata ya Kikuyu Kusini, Anselim Kutika, akizungumza kuhusu tukio hilo alisema nyuki hao walikuwa wamerundikana katika shimo lililopo chini ya mti, jirani na nyumbani kwa marehemu ndipo watoto waliokuwa katika sherehe hizo kuanza kuwachokoza kwa kutumia fimbo.

“Kutokana na watoto hao kuwachokonoa nyuki hao walianza kushambulia watu waliokusanyika eneo hilo na kumwelemea mzee huyo na kumsababishia kifo.

Zaidi ya watu saba wameshambuliwa na nyuki hao watoto kwa wakubwa,” alisema Kutika.

“Naomba wakazi wa maeneo mbalimbali katika mtaa huu kuwa makini na suala la nyuki wanaojenga katika makazi ya watu huweza kushambulia watu na kusababisha vifo.”

Alisema wameshatoa taarifa kwa Ofisa nyuki ambao tayari wameshughulikia suala hilo ikiwamo kupulizia dawa ili wasiendelee kuwadhuru watu katika maeneo hayo.

Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Martine Otieno, alisema tukio hilo bado halijamfikia ofisini kwake huku akitoa tahadhari jamii inapaswa kuwa makini na pale wanapoona sehemu kuna vitu hatarishi wanapaswa kutoa taarifa sehemu husika.

# Wananchi 9,799 walipwa fidia kupisha mradi boma la mafuta

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WANANCHI 9,799 kati ya 9,898 sawa na asilimia 98.8 wamelipwa fidia na serikali Sh. bilioni 34 kwa ajili ya kupisha mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Chongoleani mkoani Tanga hadi Hoima nchini Uganda.

Mratibu wa kitaifa wa mradi huo, Asiadi Mrutu aliyasema hayo wakati wa kikao kazi cha wataalam cha kujadili kuhusu kuanza la upimaji mkuza wa bomba hilo kinafanyika wilayani humo.

Mrutu alisema hivi sasa shughuli mbalimbali zinaendelea katika maeneo ya kipaumbele ni kuandaa makambi ya ujenzi, karakana ya kuwekea mabomba eneo la Sojo na ujenzi wa jengo umekamilika kwa asilimia 100 na kunafungwa mtambo wa kuandaa mabomba ili yasiweze kupata joto wakati wa kusafirisha mafuta.

Alisema katika kambi namba 11 ambayo ipo Kijiji cha Ntondo, mkoani Singida, maandalizi yamekamilika kwa asilimia 100 na anasubiriwa mkandarasi mkubwa wa ujenzi wa bomba hilo aanze kazi rasmi.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akifungua kikao hicho aliwataka wananchi katika mikoa linalopita bomba hilo kuwa na moyo wa kizalendo kwa kuruhusu mradi kutekelezwa bila vikwazo vyovyote hasa vya ardhi.

Alisema kuanza kazi kwa hatua mbalimbali za mradi wananchi wamenufaika kupitia fursa mbalimbali na serikali ina imani kazi inayoendea kuanza itazalisha fursa zaidi kwa jamii.

“Serikali imedhamiria kuhakikisha miradi yote ya kimkakati inakamilika kwa muda uliopangwa na hili linajidhihirisha kwa ninyi wataalamu ambao mnaonekana kuwa na nia ari itakayowapa msukumo wa kukamilisha kazi iliyopo mbele yenu kwa weledi mkubwa ili kupata matokeo chanya,” alisema.





# Halmashauri yafunga vyoo kukosa huduma ya maji

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

UONGOZI wa Kituo cha Afya cha Ilembo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, umevifunga vyoo kutokana na tatizo la ukosefu wa maji ya uhakika kituoni hapo.

Aidha, inadaiwa kuwa asilimia kubwa ya wananchi wa eneo hilo hawana elimu ya kutosha kuhusu matumizi sahihi ya vyoo hivyo hali ambayo imekuwa ikisababisha kuwa vichafu na kuhatarisha afya za watumiaji.

Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Dk. Philimon Urungi, aliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya wawakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), wanaosimamia mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya maji na usafi wa mazingira (SAWA).

Alisema mfumo wa maji katika kituo hicho umeharibika na kusababisha yasifike kwenye vyoo hivyo hali ambayo inavifanya kuwa vichafu.

Alisema wakati wanaendelea na taratibu za kurekebisha mfumo huo wa maji waliamua kuvifungua vyoo vya shimo ambavyo ndivyo vilikuwa vinatumika kabla ya kuvijenga vya kisasa.

"Vingine vina mwaka mmoja sasa havitumiki na vingine miezi mitatu, lakini pia tulibaini kwamba wananchi hawana elimu ya kutosha kuhusu matumizi ya vyoo hivi vya kisasa, wanajisaidia hata kama hakuna maji," alisema Dk. Urungi.

Ofisa Mazingira wa kituo hicho, John Mwaijulu, aliiomba serikali kuwapeleka wataalamu vijijini kwenda kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi sahihi ya vyoo hivyo ili kuondokana na tatizo linalowakabili.

Alisema hata maji yakiwekwa kwenye ndoo ndani ya vyoo hivyo, baadhi ya wananchi wanayatumia kwa shughuli zingine ikiwamo kufulia jambo ambalo siyo sahihi.

Vilevile, alisema baadhi yao wanaziondoa ndoo hizo kwenye vyoo na kwenda kuzitumia nje.

"Sasa wapo ambao wakiingia chooni na kukuta ndoo hazipo, wanajisaidia hivyohivyo na kuacha vinyesi hali inayosababisha mazingira kuwa machafu, ni vyema serikali ikatusaidie kutoa elimu kwa wananchi," alisema Mwaijulu.

Mwenyekiti wa Kamati ya kituo hicho, Asumwise Mwakalindile, alikiri wananchi wa eneo hilo kutokuwa na elimu kuhusu matumizi ya vyoo hivyo vya kisasa. Alisema katika maeneo hayo wananchi wamezoea kutumia vya shimo na kwamba teknolojia ya vyoo vya maji ni ngeni kwao na kuhitaji elimu ya kutosha ili wavitumie kwa usahihi.

Msimamizi wa Mradi wa SAWA, Joachim Asenga, aliahidi kushirikiana na uongozi wa kituo hicho kurejesha mfumo wa maji ulioharibika ili huduma hiyo iendelee kupatikana bila tatizo wakati tatizo la elimu likiendelea kushughulikiwa.

Alisema walibaini kuwa upatikanaji wa fedha za kituo hicho ni mdogo wanaweza wakatumia muda mrefu kurekebisha mfumo huo na kwamba wadau watatoa fedha baada ya kupewa mchanganuo wa vituo vinavyohitajika na gharama.

"Lakini pia tutashirikiana na wenzetu wa halmashauri kuziongezea nguvu serikali za mitaa kwenye utoaji wa elimu, elimu ni silaha muhimu zaidi," alisema Asenga.

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ilembo, Mtera Mwaruwanda, alisema wataitumia mikutano ya hadhara na mikusanyiko mbalimbali kutoa elimu kwa matumizi sahihi ya vyoo.



Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia watoto (UNICEF) anayesimamia mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya maji na usafi wa mazingira (SAWA), Edwin Kalugendo, akifundisha wanafunzi namna ya kunawa mikono wa Shule ya Msingi Ilindi kwenye miundombinu iliyojengwa na shirika hilo shuleni hapo wilayani Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## NFRA kununua mpunga, mahindi kuwapa wakulima soko

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

SERIKALI kupitia Wizara ya Kilimo imetoa Sh. bilioni 50 kwa Wakala wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kwa ajili ya kununua mpunga na mahindi katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya ili kuwasaidia wakulima kupata soko la mazao yao.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliyasema hayo alipozindua ununuzi wa mpunga wa wakulima katika ghala la NFRA lililoko katika Kijiji cha Uturo kilichopo Kata ya Mapogoro, wilayani Mbarali.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 37 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa mpunga na Sh. bilioni 13 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa mahindi.

Alisema wanakusudia kununua tani zaidi ya 31,000 za mpunga na tani 14 za mahindi katika Mkoa wa Mbeya pekee na kuwataka wakulima kujitokeza kuuza mazao hayo kwenye vituo vilivyoainishwa.

"Wataalamu watawafuata hukohuko, sasa hivi wapo hapa Uturo wakitoka hapa watakwenda Kapunga, watakwenda Ubaruku mpaka Madibira watafika, kwahiyo nawaomba wananchi changamkieni fursa hii," alisema Homera.

Alisema lengo la kununua mazao hayo ni kuweka akiba kwa ajili ya kukabiliana na uhaba wa chakula kwa kuwa chakula hicho kitasambazwa kwenye maeneo ambayo yatakuwa na uhaba wa chakula ndani na nje ya nchi.

Aliwaagiza maofisa wa NFRA kuwalipa mapema wananchi wanaopeleka mazao yao kwenye vituo ili kuepuka migogoro na wananchi.

Meneja wa NFRA Kanda ya Songwe ambayo inahudumia mikoa ya Mbeya na Songwe, CPA Eva Kwavava, alisema wananunua mpunga huo kwa bei ya Sh. 1,100 kwa kilo kwa kuwa ndiyo bei ya soko kwa sasa.

Alisema wameamua kununua mazao hayo kwa kuweka vituo katika maeneo mbalimbali ili kuwasogezea huduma wananchi kwenye maeneo yao na kuwaondolea usumbufu wa kutumia gharama kubwa kusafirisha.

"Haya mazao tunakwenda nayo sambamba, huku tunanunua mpunga, lakini maeneo mengine tunaendelea kununua mahindi, kwahiyo tunanunua mazao haya kwa bei iliyopo sokoni ili tupate mazao mengi," alisema Eva.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali mstaafu, Denis Mwila alisema NFRA hawajaanza kununua bei ya mpunga ilikuwa Sh. 80,000 kwa gunia la kilo 100, lakini kwa sasa bei imepanda na kufikia Sh. 110,000.

Alisema kutokana na hali ilivyo kuna uwezekano bei ikaendelea kupanda zaidi hasa endapo wanunuzi wengine wataamua kushindana na serikali kwa kuamua kununua kwa bei ya juu zaidi. Aliwataka wakulima wa wilaya hiyo kuendelea kuongeza juhudi kwenye kilimo kutokana na serikali kuendelea kuboresha mazingira ya kilimo hasa kwa kutoa ruzuku kwenye pembejeo.

Baadhi ya wakulima wa Skimu ya Umwagiliaji ya Uturo waliahidi kuiuzia serikali mpunga wao kwa kuwa bei iliyopo ni nzuri na inaendana na gharama za uzalishaji.

Mmoja wa wakulima hao, Daima Kilongo alisema bei ambayo NFRA wananunulia mpunga inaashiria kwamba kilimo ni ajira kama ilivyo ajira zingine kutokana na kipato cha wakulima kuzidi kuimarika.

## Taasisi yatoa mahitaji wanafunzi wasiojiweza zaidi 600

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

TAASISI ya DIDO Mwanafunzi Initiative kwa kushirikiana na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya wametoa mahitaji ya shule kwa wanafunzi wasiojiweza 622 katika wilaya tatu za mkoa huo ili kuunga mkono jitihada za serikali kuhakikisha kila mwanafunzi anapata elimu bora katika mazingira ya utulivu.

Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Rehema Moses, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Mbeya kwenye kilele cha wiki ya ugawaji sare kwa wanafunzi wasiojiweza iliyoambatana na harambee ya kuchangia fedha kwa ajili ya wanafunzi hao kupitia kampeni ya Mvishe Aende Shule.

Rehema alisema kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa huo, wamefanikiwa kutoa sare kwa wanafunzi wasiojiweza zikiwamo taulo za kike 984, fulana kwa wanafunzi wa kiume 490, soksi kwa wanafunzi 120 pamoja na nguo za ndani kwa wanafunzi wa kike 48 na kiume 48 katika wilaya za Rungwe, Chunya na Mbarali.

"Kwa mwaka huu tunalenga kuwafikia wanafunzi 10,000 na mpaka sasa tumewafikia wanafunzi 4,796 tutaendelea kukuza wigo ili kuwafikia wanafunzi wengi wenye uhitaji na kuwasaidia wanafunzi katika safari yao ya elimu na kupunguza mzigo wa kifedha kwenye familia," alisema Rehema.

Aliongeza kuwa mbali na kutoa mahitaji hayo wanashirikiana na serikali kuongeza uelewa kwa wanafunzi ili kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia na kukatisha ndoto zao.

Alisema wanaendelea na hamasa kwa wafanyabiashara na wadau mbalimbali ili kuchangia fedha na vitu kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaotoka katika familia duni.

Akiongoza harambee hiyo Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa wito kwa jamii kusaidia wasiojiweza kwa kuwa kufanya hivyo ni sehemu ya kupata baraka huku akisisitiza serikali kuwaunga mkono, taasisi na wadau wanaosaidia serikali kukuza maendeleo kupitia sekta mbalimbali.

Homera aliahidi kutoa Shilingi milioni mbili kwa ajili ya wanafunzi wasiojiweza huku akipongeza taasisi hiyo kwa wazo lake la kusaidia wanafunzi na kwamba serikali haiwezi pekee yake kutosheleza mahitaji ya kielimu.

Aidha, zaidi ya Sh. milioni 10 zikiwa ni ahadi na fedha taslimu zilipatikana katika harambee hiyo iliyoongozwa na Mkuu huyo wa Mkoa huku akiwakaribisha wadau wengine kuendelea kuchangia kampeni hiyo kufikia malengo ya kuwasaidia wanafunzi wengine wasiojiweza.

## Serikali kuiboresha Taasisi ya Utatifi wa Afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema itaiimarisha Taasisi ya Utafiti wa Afya (ZAHRI) ili iweze kutoa taarifa za kisayansi ambazo zitasaidia udhibiti wa magonjwa kwa binadamu.

Mkurugenzi Utumishi Uendeshaji, Mwatoum Ramadhan Mussa, aliyasema hayo wakati wa mkutano wa ushirikiano kati ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Maradhi ya Binadamu (NIMR) na Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI).

Alisema katika kuimarisha taasisi ya utafiti wa afya, Wizara ya Afya itaajiri wataalamu wenye uwezo wa kufanya utafiti ili kuisaidia wizara kutatua magonjwa kutokana na utafiti utakaoandaliwa.

Alisema kuwa kutokana na ushirikiano uliopo baina ya NIMRI na ZAHRI kutawezesha kubadilishana uzoefu pamoja na kuwapatia taaluma zaidi watafiti wa Zanzibar kutokana na ujuzi mkubwa walionao wenzao wa NIMR.

Mkurugenzi Mkuu wa NIMR, Profesa Said Shebe Aboud, alisema lengo la kuja Zanzibar ni hatua ya utekelezaji wa makubaliano yaliosainiwa kwa lengo la kuimarisha masuala ya utafiti.

Alisema kuwa NIMR imepiga hatua kubwa ya utekelezaji wa kazi zao ambapo wana vituo saba kwa Tanzania na Dare es Salaam ina vituo viwili na tayari wameshafanya utafiti mbalimbali.

Alisema wataendeleza ushirikiano na Zanzibar kwa kufanya utafiti pamoja na kubadilishana uwezo kwa watendaji wa taasisi hizo ili kuweza kuleta mabadiliko katika Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar.

Akiwasilisha ripoti ya ZAHRI, Mkurugenzi Uendeshaji wa Ndani katika taasisi hiyo, Bernard Mtuta, alisema kuanzishwa taasisi hiyo kumetokana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutambua umuhimu wa upatikanaji wa taarifa za kisayansi ambazo zitasaidia kupanga mikakati mbalimbali ya tiba na udhibiti wa magonjwa.

Alisema licha ya ZAHRI kukabiliwa na uhaba wa wafanyakazi wamewezesha kufanya utafiti mbalimbali kwa kushirikiana na taasisi nyingine ambapo wameweza kufanya utafiti zikiwamo za kuangalia hali halisi ya maradhi ya ngozi Micheweni Pemba, utafiti wa miongozo ya jamii kuhusiana na UVIKO-19 pamoja na kupata maoni ya wananchi kuhusiana na ugonjwa huo.

Alisema taasisi inaendelea kufanya utafiti mbalimbali ikiwamo ya ongezeko la thamani ya dawa za miti shamba, utafiti wa kujua sababu na viashiria vya ugonjwa wa figo kwa wananchi wa Zanzibar.

# Dk. Mwinyi: Walimu watakaofaulisha wanafunzi vizuri tutawapa zawadi

**Na Mwandishi wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema itawahamasisha walimu wa shule za serikali kwa kuwapatia zawadi kadri watakavyotoa ufaulu wa daraja la juu kwa wanafunzi wanaowasimamia kwenye masomo yao.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi aliyasema hayo kwenye hafla ya kuwazawadia kompyuta aina ya "laptop" wanafunzi wa kidato cha nne na sita waliofanya vizuri kwenye mitihani yao ya taifa.

Alisema walimu wanahitaji motisha maalumu ili kuboresha mfumo wa elimu Zanzibar kwa kuleta mageuzi makubwa kwenye sekta hiyo ikiwamo kuongeza ufaulu mzuri.

Dk. Mwinyi alisema serikali imejikita kwenye kuimarisha miundombinu kwa shule zote ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi wengi kwa kuendelea kujenga shule za ghorofa za msingi na sekondari ili kutoa nafasi kwa wanafunzi kuhudhuria masomo ya madrasa wakati wa jioni kwa kuwa na mkondo mmoja.

Akizungumzia ufaulu wa wanafunzi, Dk. Mwinyi alisema mara zote amekua akiwaahidi zawadi nzuri zaidi kwa wanafunzi hao kama hamasa ya kuwashajihisha wengine kufanya vizuri hali aliyoieleza kuleta tija katika kuongeza ufaulu nchini.

Alisema adhma ya serikali ni kuondoa ufaulu wa daraja sifuri na daraja la nne kwa kuweka mkazo kwenye kuongeza ufaulu zaidi.

Naye Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulgulam Hussein, alisema wizara imeongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa sekondari kutoka asilimia 4.6 mwaka 2021 hadi kufikia 26 kwa mwaka 2023, hali aliyoitaja mafanikio makubwa kwa sekta ya elimu na kueleza kuwa hamasa zimesaidia kuongeza ufaulu huo.



Diwani wa Kata ya Misozwe wilayani Muheza mkoani Tanga, Jestina Mntangi (kulia), akishukuru baada ya kupokea msaada wa baiskeli kutoka kwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Muheza, Hamis Mwinjuma, wilayani humo juzi. Mbunge huyo, alitoa baiskeli mpya 210 kwa ajili ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika kata 37 za jimbo hilo, ili kuwapunguzia mwendo wa kutembea umbali mrefu kwenda shuleni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wanne mbaroni tuhuma kutapeli wananchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATU wanne wamekamatwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja kwa tuhuma za utapeli katika maeneo yanayotoa huduma za kifedha Zanzibar.

Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, ACP Richard Thadei Mchomvu, akizungumza na vyombo, alisema Juni 19 mwaka huu majira ya saa 4:00 asubuhi nje ya Benki ya CRDB tawi la Zanzibar lililopo Michenzani Mall watuhumiwa wanne walimtapeli mwananchi Sh. milioni 10.

Alisema baada ya uchunguzi kupitia CCTV kamera walifanikiwa kuitambua gari lililotumika katika utapeli huo yenye namba za usajili Z.971 HZ aina ya Alfard yenye rangi nyeupe.

Aidha, alisema baada ya kuendelea na upelekezi mtuhumiwa mmoja aliyefahamika kwa Masoud Ali Suleiman (48) mkazi wa Fuoni ambaye ni dereva wa gari hiyo alikamatwa ambaye alishirikiana na watuhumiwa wengine watatu kufanya utapeli huo.

"Baada ya mahojiano alikiri kufanya tukio hilo na kueleza kwamba washiriki wengine watapatikana kwani walikuwa na lengo la kufanya tena tukio hilo la utapeli jijini Zanzibar," alisema.

Alisema katika msako huo walifanikiwa kuwakamata wahalifu watatu wakitokea jijini Dar es Salaam wanaojihusisha na utapeli wa kuibia watu kwa kutumia mbinu ya kuwahadaa kwa noti za dola bandia katika maeneo ya benki na maeneo mingine.

Kamanda Mchomvu alieleza kuwa watuhumiwa walikamatwa wakiwa na dola bandia zilizohifadhiwa ndani ya mfuko wa rangi ya bluu.

Aliwataja watuhumiwa waliokamatwa kuwa ni Yakoub Joseph Yakoub (28), Michael Msunga Gonald (50) wote wakazi wa Kinondoni na Yarem Badru Athumani (48) mkazi wa Temeke jijini Dar es salam. "Utapeli huu hawaufanyi hapa kwetu tu bali pia wanakwenda na mikoa mengine ikiwamo ya Arusha, Mwanza, Dodoma na Dar es Salaam na baada ya mahojiano walikiri kweli kwamba wanafanya utapeli huo," alisema.

Hata hivyo alisema kwa sasa mahojiano yanaendelea ili kubaini mtandao huo na matukio ya utapeli katika huduma za kifedha ambako yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara katika vituo vya polisi.

Aidha, alisema Jeshi la Polisi linawataka wananchi kutoa taarifa haraka pindi wanapoona viashiria vya kitapeli ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahalifu hao.

Pia aliwataka wananchi kuhakikisha wanapata huduma katika vituo sahihi vya kibenki ili kuepuka kutapeliwa.



Watuhumiwa wa kosa la wizi wa fedha zaidi ya Sh. bilioni moja za Benki ya NMB, wakitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, kusikiliza mashtaka yanayowakabili. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Miamala ya simu yaongezeka, tozo zapungua kwa bilioni 4/-

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

IDADI ya miamala ya fedha kupitia mitandao ya simu imeongezeka kwa asilimia 24 huku tozo za miamala hiyo zikipungua kwa asilimia 22.99 ndani ya mwaka mmoja.

Vilevile, lugha ya Kiswahili imetajwa kuongeza watumiaji wa intaneti ndani ya mwaka mmoja kwa asilimia 17 kutokana na kuwapo maudhui ya Kiswahili katika intaneti.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya mamlaka kwa mwaka 2022/23 na maendeleo ya sekta ya mawasiliano nchini, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri Bakari, alisema kwa kipindi cha Juni 2022 miamala ilikuwa bilioni 3.76 na hadi kufikia Juni 2023 ilikuwa bilioni 4.67 sawa na ongezeko la asilimia 24.

Alisema tozo za miamala zimepungua kutoka bilioni 19.2 mwezi Julai 2022 hadi kufikia bilioni 14.8 mwezi Juni 2023, sawa na asilimia 22.99.

"Kupungua kwa tozo ya miamala ya fedha kumesababishwa na kupungua kwa viwango vya tozo ya miamala ya fedha vilivyoanza kutumika Oktoba Mosi 2022," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema takwimu zinaonyesha kuongezeka kwa watumiaji wa intaneti kwa asilimia 17 kutoka watumiaji milioni 29.1 mwezi Julai 2022 hadi kufikia milioni 34.04 kwa mwezi Juni 2023.

"Sababu kuu zinazochangia ongezeko la matumizi ya intaneti zimeendelea kuwa ni kuwapo maudhui ya Kiswahili katika intaneti ikijumuisha kuongezeka kwa programu timizi kwa lugha ya Kiswahili," alisema.

Kuhusu usajili wa laini za simu, alisema ndani ya mwaka mmoja zimesajiliwa laini milioni 7.3 na kuongeza idadi kutoka milioni 56.7 kwa mwezi Julai 2022 hadi kufikia milioni 64.1 Juni 2023 sawa na ukuaji wa asilimia 13.

"Takwimu zinaonyesha mikoa mitano Tanzania inayoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya laini za simu zinazotumika hadi Juni 2023 ni Dar es Salaam (laini 11,797,554), Mwanza (laini 4,246,212), Arusha (3,858,283), Mbeya (3,687,622) na Dodoma (3,421,006)," alisema.

Akizungumza kuhusu usimamizi wa usalama mtandaoni, mkurugenzi huyo alisema hadi kufikia Juni 2023 kulikuwa na mashauri 812 ya usalama mtandaoni kulinganishwa na mashauri 920 kwa kipindi cha mwaka 2021/22.

Hata hivyo, alisema gharama za kupiga simu ndani na nje ya mtandao zimekuwa na uelekeo wa aina moja na kukaribiana sana, hivyo kumwezesha mteja kuwa na uhuru wa kupiga simu popote.

"Mwenendo wa gharama ndani na nje ya mtandao ndani ya kifurushi zimeendelea kushuka na kukaribiana na hali hii imechochea shughuli nyingi za kiuchumi kuweza kufanyika kupitia mawasiliano ya simu kulinganisha na hapo awali," alisema.

Pia alisema uwiano baina ya mitandao na matumizi unaonyesha maeneo mengi yamefikiwa na huduma za intaneti lakini watumiaji ni wachache.

"Sababu ni idadi ndogo ya watumiaji wenye simu janja, hivyo kupelekea kuwapo na umuhimu wa TCRA kufuatilia kwa kina gharama za simu janja na pia mwelekeo wa kufikia lengo la serikali la asilimia 80 ya watumiaji wa huduma za intaneti kufikia mwaka 2025,"alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kumekuwa na mwamko wa kutoa taarifa ya uhalifu wa mitandaoni ambapo katika robo ya tatu ya mwaka 2022/23, idadi ya majaribio ya uhalifu yaliyorekodiwa ni 12,044 na kwa robo ya nne ya mwaka huo ni majaribio 23,084.

**VIPINDI VYA MAADILI**

Mkurugenzi huyo pia alisema katika jitihada za kujenga jamii ya kitanzania yenye maadili mema, vituo 14 vyenye leseni ya kitaifa vinarusha vipindi vya kutoa elimu ya malezi bora ya familia na vijana.

"TCRA kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inaratibu programu maalum ya kuandaa vipindi vya maadili vitakavyorushwa vituo 150 vyenye leseni kiwilaya," alisema.

**VIPAUMBELE 2023/24**

Mkurugenzi huyo pia alisema TCRA itahamasisha uanzishaji wa vikundi vya kidigitali shuleni na vyuoni ili kujenga uwezo wa TEHAMA kwa wanafunzi na kuimarisha upatikanaji wa mawasiliano ya redio nchini.

## 'Jumuiya kimataifa iweke nguvu kusaidia Afrika athari UVIKO-19'

**Na Benny Mwaipaja, NEW YORK**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dk. Natu El-maamry Mwamba, amesema kuna haja Jumuiya ya Kimataifa kuweka nguvu ya pamoja kulisaidia Bara la Afrika kukabiliana na changamoto mbalimbali zitokanazo na athari za Uviko-19, mabadiliko ya tabianchi na mizozo ya kivita.

Amesema mambo hayo matatu yanatishia ustawi wa nchi mbalimbali kiuchumi na kijamii na kukwamisha kasi ya utekelezaji wa ajenda ya Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

Jijini New York, Marekani jana, Katibu Mkuu alitoa rai hiyo wakati akihutubia wajumbe wa Jukwaa la Juu la Siasa la Umoja wa Mataifa kwa niaba ya Umoja wa Afrika, ambapo Tanzania ni Mwenyekiti wa Umoja huo kwa mwaka 2023.

Dk. Mwamba alisema changamoto hizo zimekuwa kikwazo katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na kuwasukuma watu wengi katika lindi la umaskini na kutaka hatua madhubuti na za haraka zichukuliwe kukabiliana na hali hiyo.

Alisema Bara la Afrika limejaliwa kuwa na rasilimali nyingi za jua, upepo, maji na jotoardhi na kutolea mfano wa nishati jua ambayo ina uwezo wa kuzalisha umeme wa terawatts 10 unaoweza kutosheleza mahitaji na kuwawezesha upatikanaji wa nishati safi itakayookoa mazingira.

"Katika uhusiano huu, Bara la Afrika linasisitiza umuhimu wa kuhakikisha nishati safi na nafuu kwa wote inapatikana ambapo hamasa ya uwekezaji zaidi inahitajika katika maeneo mengi, ikiwa ni pamoja na uwekezaji kidigitali, teknolojia bunifu na sekta nyingine muhimu," alisema.

Dk. Mwamba alisema uwekezaji katika sekta ya majisafi na salama pamoja na usafi wa mazingira mijini na vijijini ni suala muhimu ili kujenga jamii yenye afya na ustawi na kuitaka Jumuiya ya Kimataifa kuweka kipaumbele katika mipango inayolenga kuimarisha huduma hiyo ya maji kwa wananchi.

Kuhusu viwanda, Dk. Mwamba alisema sekta hiyo ni muhimu kwa ajili ya kukuza uzalishaji wa bidhaa na huduma na kuwa chanzo cha ajira ya uhakika hususani kwa vijana, hivyo akatoa wito kwa mashirika na kampuni mbalimbali za kimataifa kuwekeza mitaji na teknolojia barani Afrika.


**KUPOTEA KWA CHETI**



HUSSEIN ALLY HUSSEIN anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: S.2426/0056 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia CHAMAZI ISLAMIC SEMINARY mwaka 2011. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
DAR/URA/RB/240518/2023

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**EDINESTA NICOLAUS MSEMWA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA **IST** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T. 640 DSC** RANGI YA SILVER.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/240060/2023**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

EBENEZA RINGAWAFO NKYA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA LANDCRUISER yenye usajili namba T582 AKQ. Kwa yeyote atakaeona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
ARU/ARU/RB/241314/2023

# Russia yakataa kurefusha mkataba usafirishaji nafaka

**MOSCOW,** RUSSIA

RUSSIA imekataa kurefusha mkataba wa usafirishaji wa nafaka huku msemaji wa Rais Vladimir Putin, Dmitry Peskov, akisema kwamba nchi hiyo itarudi kushiriki mkataba huo mara tu matakwa kuhusiana na usafirishaji wa nafaka na mbolea zake yatakapotimizwa.

Ilielezwa kuwa Ikulu ya Kremlin inataka hasa vikwazo vilivyowekwa na mataifa ya Magharibi kuhusiana na masuala ya malipo, usafirishaji na bima viondolewe.

Hata hivyo, Marekani na nchi za Magharibi wamepinga madai hayo ya Russia wakisema vikwazo vyao havilengi nafaka na mbolea za taifa hilo.

Aidha, uamuzi huo wa Russia kujitoa kwenye mkataba wa kusafirisha nafaka za Ukraine kupitia bandari za Bahari Nyeusi umezusha wasiwasi wa kimataifa, huku viongozi kadhaa ulimwenguni wakijitokeza kuzungumzia athari zinazoweza kuikumba dunia iwapo shehena ya nafaka itazuiwa na usambazaji wa chakula kutetereka.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) Antonio Guterres, alisema kwamba amevunjwa moyo sana kwa kuwa barua aliyomtumia Rais Putin wiki iliyopita, iliyokuwa na mapendekezo ya mikakati ya

kuunusuru mkataba huo, haikuzingatiwa.

Guterres, alisema mkataba huo ambao ulifika mwisho rasmi juzi Jumatatu, ulikuwa ni tumaini la usalama wa chakula duniani na matumaini pia katika ulimwengu ulio na matatizo chungumzima.

Rais wa Uturuki, Reccep Erdogan, ambaye alikuwa na dhima kubwa katika kutiwa saini kwa mkataba huo, alisema anahisi kwamba Rais Putin ana nia ya kurudi kwenye mkataba huo.

Erdogan alisema atafanya mazungumzo na Putin kuelekea ziara yake inayosubiriwa kwa hamu nchini Uturuki mwezi Agosti.

Naye Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy, aliibua uwezekano wa kurudia usafirishaji wa nafaka bila ushiriki wa Russia, akisema Ukraine itaomba usaidizi wa Uturuki, ili kuhakikisha kwamba vizuizi vilivyowekwa na Russia mwaka jana, havitekelezwi.

Katika maoni yaliyosambazwa kwenye mitandao ya kijamii na msemaji wake, Seriy Nykyforov, Zelensky alisema hata bila ya shirikisho la Russia, kila kitu kinapaswa kufanywa ili waweze kutumia njia ya Bahari Nyeusi.

Zelensky aliongeza kuwa hawaogopi na kwamba kampuni za usafirishaji zimewafuata na ziko tayari kuendelea na usafirishaji.

Katika hatua nyingine, Rais wa Halmashauri Kuu ya Umoja wa Ulaya Ursula von der Leyen, alisema uamuzi wa Russia wa kuahirisha mkataba huo wa usafirishaji nafaka ni hatua isiyokuwa na maana na kwamba umoja huo utaendelea kufanya kazi katika kuhakikisha usalama wa chakula kwa nchi maskini.

**Hata hivyo, Marekani na nchi za Magharibi wamepinga madai hayo ya Russia wakisema vikwazo vyao havilengi nafaka na mbolea za taifa hilo.**

Waziri wa mambo ya nje wa Ujerumani, Annalena Baerbock, aliyekuwa mjini New York, alimtaka Rais Putin kuacha kutumia njaa kama silaha katika uvamizi wake, kwa ajili ya kupatikana amani duniani.

Shashwat Saraf ni mkurugenzi wa dharura Afrika Mashariki katika Shirika la Kimataifa la Uopoaji (IRC) alisema athari ya Russia kutourefusha mkataba huo zitakuwa kubwa Somalia, Ethiopia na Kenya, nchi ambazo zimekabiliwa na kiangazio kikali kuwahi kushuhudiwa katika eneo la Pembe ya Afrika katika miongo kadhaa.

Ukraine na Russia ni miongoni mwa wauzaji wakubwa wa nafaka na bidhaa zingine za chakula duniani na utatizaji wa aina yoyote wa usafirishaji huo unaweza kusababisha kupanda kwa bei za chakula kote duniani. **DW**

## EAC kuchunguza mauaji ya raia Kivu

**KINSHASA,** DRC

UJUMBE kutoka vikosi vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) nchini

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), unatarajiwa kwenda jimboni Kivu Kaskazini Mashariki, kufanya tathmini ya kilichotokea baada ya ripoti za kuuawa kwa watu 11 na waasi wa M23.

Licha ya Kundi la M23 kukanusha kuhusika na mauaji hayo, vyanzo katika eneo la Rutshuru vilisema miili ya watu 11 waliopigwa risasi na kukatwakatwa iligunduliwa siku mbili zilizopita huko Bukombo, karibu

kilomita 100 kaskazini mwa mji mkuu wa Goma, baada ya kuripotiwa mapigano kati ya waasi hao na makundi ya wapiganaji wenye silaha.

Shirika linalofuatilia mizozo katika eneo hilo la Kivu Security Tracker (KST), limefahamisha kuwa watu hao waliuawa baada ya kulazimishwa kubeba mizigo ikiwamo zana za kijeshi, na kwamba kundi la M23 ndilo linaloshukiwa kuwa wahusika wa mauaji hayo.

Msemaji wa kikosi cha EAC Meja Albert Nyakundi, alisema timu ya kutafuta ukweli kuhusu kilichotokea kabla ya mauaji hayo, inajiandaa kusafiri hadi eneo hilo ili kufahamu zaidi nini hasa kilitokea na nani alihusika. **RFI**



Waasi wa M23 wanaoripotiwa kuendelea kutekeleza mashambulizi dhidi ya raia Kaskazini Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), licha ya kutakiwa kusitisha mapigano. **PICHA: AFP**

## Wimbi la joto laendelea kuikabili Ulaya

**SARDINIA,** ITALIA

WIMBI la joto linaendelea kote kusini mwa Ulaya, huku hali joto katika eneo la kati la Mediterania ikitarajiwa kuongezeka, jambo linaloendelea kuwaweka katika hali tete wananchi barani humo.

Ilielezwa kuwa kisiwa cha Italia cha Sardinia kinatarajiwa kushuhudia joto la juu la nyuzi jato 46 mchana, huku kukitolewa onyo kwamba joto kali linaweza kuendelea kwa siku 10 zaidi katika sehemu za Italia.

Pia ilibainishwa kuwa katika mji mkuu wa Roma, halijoto inaweza kubaki juu ya nyuzi joto 40 kwa siku 15.

Uhispania pia imekabiliwa na mawimbi ya joto mfululizo, huku halijoto jana ikifikia nyuzi joto 44 kusini mwa nchi hiyo.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa kumekuwa na moto katika kisiwa cha Uhispania cha La Palma na Ugiriki bara kwamba kumekuwa na ripoti za kukatika kwa umeme katika baadhi ya maeneo huku mahitaji yakiongezeka kwa sababu ya viyoyozi.

Aidha, taarifa zinaeleza kuwa nchi nyingi katika ulimwengu wa kaskazini zimefikia viwango vya joto vilivyovunja rekodi, katikati ya msimu wa joto usio wa kawaida wa kiangazi.

Huko Asia, vyombo vya habari vya ndani viliripoti kwamba angalau watu 60 nchini Japan walitibiwa kutokana na joto kali, na wengi wao walipelekwa hospitalini.

Sehemu za China pia zinakabiliwa na joto la juu, ikiwa ni pamoja na eneo la Xinjiang, zikifuatiwa na Amerika ya Kaskazini na Ulaya.

Hali ya hewa ya joto pia inatarajiwa kuongezeka barani Ulaya wiki hii, huku wimbi la joto katika Amerika ya Kaskazini likitabiriwa kuendelea hadi wiki ijayo. **BBC**

HABARI MICHEZO

# SIMBA YAWEKA NGUVU KWA KIPA MCAMEROON

**Na Adam Fungamwangwo**

KLABU ya Simba iko kwenye mazungumzo ya kumsajili golikipa Simon Omossola wa FC Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo raia wa Cameroon, baada ya kuachana na mpango wa kumsajili Mbrazil Caique da Santos.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa mabosi wameamua kumgeukia kipa huyo ambaye ameshawahi kuitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Cameroon, akizichezea pia Klabu ya Cotonsport ya Cameroon mwaka 2015 hadi 2020, AS Vita Club 2022 na msimu uliopita akiichezea FC Lupopo.

Chanzo chetu kimesema kuwa kipa huyo ndiye amekuwa chaguo la klabu hiyo kutokana na mabosi wengi kumfahamu na wameshawahi kumshuhudia akifanya vitu vyake langoni na moja ya mechi ilikuwa ni Aprili 5, 2021, akiichezea AS Vita Club kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Simba iliposhinda mabao 4-1 mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tunafanya mazungumzo na kipa huyo, ni mzuri na bahati nzuri tumeshawahi kumuona, mrefu futi sita na ameshaitwa mara kadhaa kikosi cha Timu ya Taifa cha Cameroon, tena chini ya kipa bora kwa sasa Andre Onana, ile kuitwa tu pekee yake kwenye nchi hiyo yenye makipa wengi wazuri inaonyesha uwezo wake," kilieleza chanzo hicho.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amekiri kuwa wapo kwenye hatua za mwisho kumalizana na kipa kutoka nje ya nchi ambaye hakumtaja jina.

"Tupo katika dakika za mwisho kumalizana na golikipa mkubwa ambaye muda si mrefu na yeye ataelekea Uturuki kungana na wenzake, tunawahakikishia wanachana na mashabiki wa Simba ni mzuri, klabu yetu ndiyo mara zote huwa na makipa wazuri mno ndani na nje ya nchi, tumeshawahi kuwa na kina Athumani Mambosasa, Omari Mahadhi, Idd Pazi, Mohamed Mwameja, Mrundi Mackenzie Ramadhani, Juma Kaseja na sasa tunaye Aishi Manula, kwa hiyo lazima tulete kipa ambaye ama ana kiwango kama Manula au kumzidi, vinginevyo ni kujipotezea muda," alisema Ahmed.

Taarifa zinaeleza viongozi wa Simba waliamua kubadili gia angani na kuachana na mpango wa kumsajili Caique baada ya kugundua kipa huyo anazungumza zaidi Kireno, hivyo wamedai itakuwa ngumu kufanya mawasiliano na mabeki wake mara kwa mara ambao ni Shomari Kapombe na Mohamed Hussein 'Tshabalala' ambao wanaongea zaidi lugha ya Kiswahili na Kingereza kidogo, pamoja na Henock Inonga na Che Fondoh Malone ambao wanazungumza zaidi Kifaransa.

Kipa huyo mwenye urefu wa futi sita na inchi mbili, anatarajia kuchukua nafasi ya Aishi Manula ambaye aliumia mwishoni mwa Ligi Kuu msimu uliopita na kufanyiwa operesheni hivi karibuni, huku taarifa zikieleza kuwa atakuwa nje ya dimba kwa zaidi ya miezi minne.

Kwa sasa Simba ipo kambini Uturuki ikiwa na makipa wawili tu, Ally Salim ambaye alidaka mechi za mwisho za Ligi Kuu pamoja na robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, pamoja na Ahmad Feruzi Teru, aliyepandishwa kutoka timu ya vijana chini ya miaka 20.

**'MWALI'...**



Baadhi ya mashabiki na wapenda soka wa Mkoa wa Mwanza wakipiga picha na Kombe la Ligi Kuu ya NBC ikiwa ni sehemu ya utaratibu wa Benki ya NBC ambayo ni Mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, kuwapelekea wateja wake pamoja na mashabiki wa soka kombe hilo na kuwapa fursa ya kuliona na kupiga nalo picha. **MPIGA PICHA WETU**

## Minziro aanza kusuka 'pira gwaride' Prisons

**Na Adam Fungamwangwo**

KOCHA mpya wa Prisons, Fred Felix Minziro, juzi alianza kwa mara ya kwanza kibarua chake cha kukinoa kikosi hicho baada ya kuachana na Geita Gold akiomba ushirikiano kwa wachezaji na viongozi, na kufafanua kuwa hiyo ndiyo silaha kubwa ya ushindi, huku akiahidi kutengeneza timu itakayocheza soka safi la kuvutia, kasi na nguvu.

Minziro aliyechukua nafasi ya Mohamed Abdallah 'Bares', ambaye alitimkia Mashujaa FC, alisema anaamini Ligi Kuu msimu ujao itakuwa ngumu kuliko ya msimu uliomalizika, hivyo inabidi afanye kazi ya ziada kukiimarisha kikosi chake.

"Ligi inayokuja ni ngumu, lakini kikubwa ni kuwa mimi nimetoka Geita Gold na ilikuwa inafanya vizuri, kwa hiyo yale yote niliyokuwa nayafanya nikiwa huko nayaleta hapa Prisons, kikubwa ni kupata ushirikiano kutoka kwa viongozi, wachezaji na mashabiki basi naamini Mungu ataleta heri zake," alisema kocha huyo akiwa jijini Mbeya.

Alisema kila mmoja anaelewa falsafa yake ya soka, na kwamba anataka kila anayekuja uwanjani kuiangalia timu yake awe ameridhika na kutojutia kiingilio chake alichotoa.

"Nataka kutengeneza timu ambayo kila mmoja akija kuiangalia ataridhika, icheze soka la kuvutia, kasi na nguvu, nataka aliyelipa kiingilio asijutie, anayetoka uwanjani timu ishinde, itoe sare au kufungwa aseme leo Prisons imepiga soka, hii ndiyo falsafa yangu," alisema beki huyo wa zamani wa Yanga na Taifa Stars miaka ya 1980.

Naye Nahodha wa timu hiyo, Jumanne El Fadhili, alisema watampa ushirikiano kocha huyo kama walivyofanya kwa walioondoka.

"Sisi tupo tayari kufanya kazi na kocha yeyote anayeletwa, kama wachezaji tumempokea na tutampa ushirikiano," alisema nahodha huyo.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Jackson Mwafulango, alisema hii ni mara ya tatu kwa Minziro kuifundisha timu hiyo.

"Tumemrudisha kwa sababu tunaamini aina ya soka ambalo Prisons tunalitaka, tunamhitaji kocha huyu," alisema Mwafulango.

## NBC na Kombe Ligi Kuu Mwanza

**Na Mwandishi Wetu**

WADHAMINI wakuu wa Ligi Kuu Tanzania Bara maarufu Ligi ya NBC, Benki ya Taifa ya Biashara(NBC), imewapelekea wakazi wa Jiji la Mwanza kombe jipya la ubingwa wa ligi hiyo namba tano kwa ubora barani Afrika.

Kwa mujibu wa NBC, lengo la kulipeleka kombe hilo mkoani Mwanza, ni kuwapa fursa wateja wa benki hiyo, wapenzi wa soka na wakazi wa jiji hilo kwa ujumla, fursa ya kulishuhudia na kupiga nalo picha.

Shughuli ya kulishuhudia kombe, imeenda sambamba na fursa ya kupata huduma mbalimbali za kibenki kwa wakazi wa jiji hilo kutoka katika benki hiyo kongwe na yenye mtandao mpana wa matawi hapa nchini.

## Wavu Taifa kutangazwa

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU za Taifa za Mchezo wa Mpira wa Wavu, zinatarajiwa kutangazwa mwishoni mwezi huu lengo likiwa ni kujiandaa na mashindano ya Mataifa ya Afrika yatakayofanyika nchini Misri na Cameroon.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Mpira wa Wavu Tanzania (Tava), Laurence Safari, alisema kwa upande wa wanawake mashindano yataanza Agosti 14, nchini Cameroon, huku ya wanaume yakianza Septemba Mosi, mwaka huu, nchini Misri.

"Tunatarajia kutangaza timu ya taifa mwishoni mwa mwezi huu ili wachezaji waingie kambini mapema kuanza maandalizi kuelekea kwenye mashindano hayo," alisema Safari.

Aidha, alisema mzunguko wa pili wa Ligi ya Taifa Mpira wa Wavu (TVNL), unatarajiwa kuanza kutimua vumbi Julai 24-30, mwaka huu katika Uwanja wa Gwambina, Dar es Salaam.

Alisema timu zote ambazo hazikupata nafasi ya kucheza kwenye mzunguko wa kwanza ndizo ambazo zitaanza kufungua pazia la mzunguko huo ambapo zitaanza kuwasili jijini Dar es Salaam Julai 23 kutoka mikoa ya Tanzania Bara pamoja na visiwani Zanzibar.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KANE HAITAKI PSG
MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, hana mpango wa kujiunga na Paris St-Germain msimu huu wa majira ya joto na mchezaji huyo wa miaka 29, anaaminika kuwa tayari kuhamia Bayern Munich, hatakubali ofa yoyote kutoka kwa mabingwa hao wa Ufaransa**. (Telegraph)**

### TONEY KUMRITHI KANE
KLABU ya Tottenham Hotspur huenda ikamnunua mshambuliaji wa Brentford, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27, ambaye anatumikia adhabu ya kutojihusisha na soka hadi Januari, ikiwa mchezaji mwenzake wa Kimataifa wa England, Harry Kane ataondoka katika klabu hiyo. **(Football Transfers)**

### MBAPPE KUKUTANA NA RAIS
RAIS wa PSG, Nasser Al-Khelaifi, atakutana ana kwa ana na mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe kwa mara ya kwanza tangu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, kutuma barua kwa klabu hiyo akisema hataongeza mkataba wake. **(Sky Sports)**

### CHELSEA KUONGEZA DAU
KLABU ya Chelsea inatarajiwa kuwasilisha dau lililoboreshwa la zaidi la pauni milioni 70 kumnunua kiungo wa Brighton, Moises Caicedo wiki hii, huku mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ecuador mwenye umri wa miaka 21, akiwa tayari ameshakubaliana na 'The Blues' hao. **(Standard)**

### RASHFORD MSHAHARA JUU
MSHAMBULIAJI wa England, Marcus Rashford, anatazamiwa kusaini mkataba mpya na Manchester United ambao unatarajiwa kumfanya alipwe mshahara wa pauni 325,000 kwa wiki. **(Times)**

### GORETZKA NA WEST HAM
KLABU ya West Ham imeungana na Manchester United kumsaka kiungo wa kati wa Bayern Munich na Ujerumani, Leon Goretzka, 28. **(Sky Germany)**

### BLOGUN AWANIWA INTER
INTER Milan inatarajiwa kutoa ofa ya pauni milioni 34.3 kwa mshambuliaji wa Marekani, Folarin Balogun, wakati wakitafuta dili la mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ambaye thamani yake ni pauni milioni 50. **(Athletic)**

### PALMER AWINDWA BRIGHTON
KLABU ya Brighton inaiongoza Burnley na Leicester City katika kinyang'anyiro cha kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa England wa chini ya miaka 21, Cole Palmer kutoka Manchester City. **(Telegraph)**

### IGOR ANUKIA BRIGHTON
BRIGHTON ipo tayari kuipiku Fulham katika usajili wa beki wa Fiorentina Mbrazil Igor mwenye umri wa miaka 25. **(Standard)**

### DIALLO AWANIWA LEICESTER
KLABU za Burnley na Leicester pamoja na Sheffield United, zina hamu ya kumnunua kwa mkopo winga wa Manchester United na Ivory Coast, Amad Diallo mwenye umri wa miaka 21. **(Mail)**

### ELVEDI ATAKIWA
KLABU ya Wolverhampton Wanderers inajadiliana kuhusu usajili wa beki wa Kimataifa wa Uswisi, Nico Elvedi, mwenye umri wa miaka 26 kutoka Klabu ya Ujerumani, Borussia Monchengladbach. **(Express & Star)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO: LIGI YA SAUDIA NI BORA KULIKO MAREKANI

**Amshangaa Messi kutua huko, pia asema kwa asilimia 100 hatarejea tena katika klabu yoyote ya Ulaya...**

**LISBON, Ureno**

MSHAMBULIAJI wa Al Nassr, Cristiano Ronaldo, amesema Ligi Kuu Saudi Arabia, Saudia Pro League, "ni bora" kuliko ile ya MLS na kwamba hana mpango wa kucheza Marekani au kurejea kwenye timu yoyote barani Ulaya.

Ronaldo alikuwa akizungumza na vyombo vya habari baada ya kucheza kipindi cha kwanza kwa Al Nassr ikichapwa mabao 5-0 na Celta Vigo ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, nchini kwao Ureno juzi.

"Ligi ya Saudi ni bora kuliko MLS," nyota huyo wa Ureno alisema alipoulizwa kuhusu kuhamia Marekani kama mpinzani wake wa zamani wa nchini Hispania, Lionel Messi, ambaye Jumapili alitambulishwa kama mchezaji mpya wa Inter Miami CF.

Ronaldo, ambaye alitolewa wakati wa mapumziko matokeo yakiwa 0-0, aliongeza: "Nilifungua njia kwa Ligi ya Saudia, na sasa wachezaji wote wanakuja hapa."

Tayari msimu huu wa majira ya joto, wachezaji kadhaa wa hadhi ya juu wamemfuata Ronaldo, huku Karim Benzema, Marcelo Brozovic, N'Golo Kante na Roberto Firmino wakisaini mikataba ya kucheza Ligi Kuu Saudia.

Mchezaji wa zamani wa Inter Milan, Milan Brozovic, alikuwa uwanjani na Ronaldo siku ya Jumatatu baada ya kujiunga na Al Nassr, Julai 3.

"Katika mwaka mmoja, wachezaji wengi wa juu zaidi watakuja Saudia. Katika mwaka mmoja Ligi ya Saudia itapita Ligi ya Uturuki na Ligi ya Uholanzi," aliongeza Ronaldo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, alielekea katika msimu wake wa kwanza kamili akiwa na Al Nassr tangu ajiunge na klabu hiyo Januari kutokana na kuondoka ghafla baada ya kuichezea Manchester United kwa mara ya pili.

Ronaldo, mfungaji bora wa muda wote wa Real Madrid, pia alisema siku zake za kucheza Ulaya zimekwisha na anaamini kiwango cha uchezaji huko kimeshuka katika miaka ya hivi karibuni.

"Nina uhakika wa asilimia 100 sitarejea katika klabu yoyote ya Ulaya," aliongeza kusema Ronaldo.

"Nina umri wa miaka 38. Na soka la Ulaya limepoteza ubora mwingi. Lililo halali na ambalo bado linafanya vizuri ni Ligi Kuu England. Wako mbele zaidi ya ligi zingine zote."

Mchezo huo pia ulikuwa wa kwanza kwa kocha Rafa Benitez kuinoa Celta Vigo ambapo pia amewahi kuzinoa Valencia na Liverpool.

Al Nassr watacheza mchezo wao wa pili wa kirafiki nchini Ureno kesho, wakimenyana na mabingwa wa nyumbani, Benfica.

## HABARI MICHEZO

# PSG MBIO MOJA NA BAYERN KWA KANE



**PARIS, Ufaransa**

PARIS Saint-Germain iko tayari kuingia kwenye kinyang'anyiro na Bayern Munich kumsajili mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, msimu huu wa majira ya joto, kwa mujibu wa ESPN.

Mapema mwezi huu, ESPN iliripoti kwamba Kane anataka kujiunga na Bayern mabingwa wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga na hayuko tayari kuongeza mkataba wake na Spurs.

Lakini PSG pia wana nia ya kumsajili nahodha huyo wa England na vyanzo viliiambia ESPN kwamba klabu hiyo imekuwa kwenye mazungumzo na kaka wa Kane na wakala wake, Charlie kwa wiki kadhaa.

Mabingwa hao wa Ligue 1 wana nia ya kuleta mshambuliaji mwingine na pia wanawafuatilia Victor Osimhen wa Napoli na Randal Kolo Muani wa Frankfurt, vyanzo viliongeza.

Kwa mujibu wa vyanzo vya habari, PSG wanaamini kwamba Kane anapendelea kwenda Bayern, lakini iwapo makubaliano hayatafikiwa, klabu hiyo ya Ufaransa itakuwa tayari kutoa fedha zaidi kwa Spurs na kujaribu kumshawishi mshambuliaji huyo kujiunga nao.

PSG wako tayari kutumia euro milioni 100 kumnunua mshambuliaji na kiasi hicho kinaweza kuongezeka iwapo Kylian Mbappé ataondoka na kujiunga na Real Madrid kwa ada kubwa ya uhamisho.

Klabu hiyo ya Ufaransa inapitia kipindi cha kuimarika baada ya Lionel Messi kuondoka na kujiunga na klabu ya MLS Inter Miami msimu huu wa majira ya joto.

Mkurugenzi wa michezo, Luis Campos ameimarisha maeneo mengine kwa kuwasajili Marco Asensio, Manuel Ugarte, Lucas Hernandez, Cher Ndour, Lee Kang-in pamoja na kocha mpya, Luis Enrique.

Bayern pia wameshuhudia ofa mbili zikikataliwa kwa Kane, lakini wanatarajiwa kutuma ofa ya tatu ya takriban euro milioni 90, ambayo bado itashindwa kufikia thamani ya Spurs.

Wakati huohuo, meneja mpya wa Spurs Ange Postecoglou alisema amezungumza na Kane, ambaye atatimiza umri wa miaka 30 Julai 28, mwaka huu, kabla ya mechi yao ya kwanza ya kujiandaa na msimu mpya dhidi ya West Ham United nchini Australia.

"Nilikuwa na mazungumzo mazuri na Harry," aliwaambia waandishi wa habari katika mkutano wake Jumatatu.

"Mazungumzo mazuri tu, nilijitambulisha, na tulizungumza zaidi juu ya klabu iko wapi na wapi anafikiria inaweza kuimarika.

"Sio maono maalum kwa mtu mmoja, ni kuhusu kundi na tumejipanga kikamilifu katika hilo - tunataka kuona timu yenye mafanikio mwaka huu."

# Rashford ajifunga mitano Man United

**MANCHESTER, England**

MARCUS Rashford amekubali kusaini mkataba mpya wa muda mrefu na Manchester United, vyanzo vimeiambia ESPN.

Mshambuliaji huyo wa England ana makubaliano ya mdomo na klabu hiyo kwa mkataba mpya wa miaka mitano ambao utamuweka Old Trafford hadi 2028.

Mazungumzo na Rashford yako katika hatua za mwisho kabla ya tangazo rasmi kufanywa.

Rashford mwenye umri wa miaka 25, ndiye mchezaji wa hivi karibuni zaidi wa United kukubali kusaini mkataba mpya katika klabu hiyo baada ya Luke Shaw na Diogo Dalot kukubaliana mapema mwaka huu.

Mkataba wa Rashford umemtia nguvu kocha Erik ten Hag anapokitayarisha kikosi chake kwa ziara ya kujiandaa na msimu



mpya nchini Marekani.

United itacheza na Lyon ya Ufaransa huko Scotland leo Jumatano kabla ya kupanda ndege kuelekea New York. Watamenyana na Arsenal huko New Jersey Jumamosi,

Rashford alikuwa sehemu muhimu ya timu ya Ten Hag msimu uliopita, akifunga mabao 30 katika mashindano yote.

Kumekuwa na nia kwa mchezaji huyo kutoka Paris Saint-Germain, lakini mshambuliaji huyo ameamua kuongeza muda wake wa kukaa katika klabu yake hiyo ya utotoni.

Ten Hag bado ana nia ya kuongeza safu yake ya ushambuliaji msimu huu wa majira ya joto kwa kusajili mchezaji mpya namba tisa.

Harry Kane wa Tottenham na Victor Osimhen wa Napoli hadi sasa wameonekana kuwa ghali sana na idara ya usajili imeelekeza nguvu zao kwa Rasmus Hojlund huko Atalanta na Randal Kolo Muani wa Eintracht Frankfurt.

## Kanote ajipanga upya Liverpool

**LIVERPOOL, England**

BEKI wa kati wa Liverpool, Ibrahima Konate amekiri anahitaji 'kuongeza kiwango' zaidi anapojiandaa kuanza msimu wake wa tatu na klabu hiyo.

Konate aliwasili hapo Liverpool kwa pauni milioni 36 msimu wa majira ya joto wa 2021 kutoka RB Leipzig.

Lakini mambo kwa Mfaransa huyo yamechukua muda - alitumia muda mwingi wa kampeni yake ya kwanza kwenye benchi, wakati majeraha msimu uliopita yalimfanya asicheze mara kwa mara.

Lakini akiwa na umri wa miaka 24, amebakiwa na miaka mitatu kwenye mkataba wake, bado kuna uwezekano mkubwa kwa Konate kuendeleza kama inavyotarajiwa.

"Nina furaha sana kuwa hapa na ninataka kushinda mataji mengi na klabu hii kwa sababu ni klabu ya ajabu yenye historia kubwa," aliiambia LiverpoolFC.com.

"Nataka kuwa sehemu kubwa ya klabu hii na kushinda mataji mengi nikiwa na klabu hii. Nadhani msimu huu, msimu wa tatu, lazima nijipange na kuonyesha haiba yangu nyingine uwanjani na maishani pia. Nina malengo mengi."



## HABARI MICHEZO

# CHILUNDA KUIBUKIA SIMBA

**Na Saada Akida**

WAKATI wakiwa wamebaki wachezaji wawili tu kujiunga kambini nchini Uturuki, uongozi wa Klabu ya Simba umeendelea kukiboresha kikosi chao kuelekea msimu mpya wa 2023/24, kwa kufanya usajili mwingine wa mchezaji wa ndani.

Tayari wachezaji wote waliosajiliwa wamewasili kambini Uturuki isipokuwa Fabrice Ngoma na Clatous Chama, ambao walitarajiwa kuondoka leo alfajiri kwenda kujiunga na wenzao kambini kujiandaa na msimu mpya.

Tayari Simba imesajili wachezaji wapya wanne wa kimataifa katika dirisha hili kubwa, ambao ni kiungo mkabaji Fabrice Ngoma raia wa DR Congo, beki Mcameroon Che Fondoh Malone, kiungo mshambuliaji Willy Essomba Onana (Cameroon) na winga Aubin Kramo (Ivory Coast).

Huku kwa upande wa wachezaji wa ndani ikiwa imekamilisha na kumtangaza beki wao pembeni wa zamani, David Kameta 'Duchu' pekee.

Hata hivyo, Simba ambayo itakuwa na kazi ngumu msimu ujao ikiwa inakabiliwa na michuano minne mikubwa, miwili ya ndani; Ligi Kuu na Kombe la FA na idadi kama hiyo kimataifa; Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi ya Soka Afrika (Africa Super League), imedaiwa kunasa saini ya mshambuliaji wa zamani wa Azam FC, Mtanzania Shaban Chilunda.

Chilunda aliachana na Azam FC baada ya mkataba wake kuisha na sasa chanzo chetu ndani ya klabu hiyo kimeliambia Nipashe kuwa amesaini mkataba wa miaka miwili kuitumikia Simba kwa msimu wa 2023/24 wa mashindano mbalimbali yaliyopo mbele yao.

Chanzo hicho makini kutoka ndani ya timu hiyo, kililiambia Nipashe kuwa, usajili wa wachezaji wazawa unaendelea na Chilunda amemalizana na Simba na muda wowote kuanzia sasa ataungana na mastaa wenzake waliopo Uturuki.

Kilisema: "Tunatambua ubora wa Chilunda, tunaamini kwa wachezaji wazawa ataongeza nguvu ndani ya kikosi, tumeshakamilisha usajili wa nyota wawili wa ndani bado tuna nafasi moja, mpango wetu ni kuongeza nguvu eneo la beki wa kati na kutokuwa na ongezeko la nyota wa kigeni."

Kuhusu idadi ya wachezaji wa kigeni ambao kwa sasa tayari wametimia 12 wanaotakiwa kwa mujibu wa kanuni za Ligi Kuu Bara, chanzo hicho kilisema, "wapo baadhi wanatarajiwa kutolewa kwa mkopo na kuuzwa kwa sababu kuna ofa ziko mezani ikiwamo ya Pape [Sakho]."

Kilisema baada ya Simba kukosa mataji misimu miwili mfululizo na kushindwa kufikia lengo la kutinga hatua ya nusu fainali Ligi ya Mabingwa Afrika, msimu ujao wanataka kufanya vizuri na kuirudisha timu kwenye ushindani kimataifa.

"Uongozi kwa ujumla haujafurahishwa na kukosa mataji yote misimu miwili mfululizo, tumeamua kukutana na kukubaliana kufanya usajili mkubwa ambao utatubeba kwenye mashindano yote tunayotarajia kushiriki," kilisema chanzo hicho.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Simba, Salim Abdallah 'Try Again', alisema hivi karibuni kuwa wanaendelea kufanya usajili mzuri na bado kuna vifaa vingine vinatarajiwa kutambulishwa.

"Wachezaji wapya wanaendelea kuwasili kambini, nawakumbusha tu hatujamaliza kusajili furaha zaidi itakuja hivi karibuni." alisema Try Again.

## SARAKASI...



Msanii wa Kikundi cha Mjomba Bendi, Mariam Mjapanizi, akionyesha uwezo wake wa kuzungusha ringi katika Maonyesho ya 18 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia (TCU), jana yanayoendelea katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Taifa Ufukweni kuingia kambini leo

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Timu ya Taifa Soka la Ufukweni (Beach Soccer), kinatarajia kuingia kambini leo kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Baraza la Vyama vya Soka Kusini mwa Afrika (COSAFA), yatakayoanza Julai 31, mwaka huu, nchini Afrika Kusini.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Boniface Pawasa, alisema mashindano mbalimbali waliyoshiriki yatasaidia kupata kikosi kipana kuelekea michuano hiyo, ambayo watashiriki kama timu alikwa.

Kocha huyo alisema maandalizi yanaendelea vema kuelekea kwenye mashindano hayo na kwamba timu itaondoka Julai 29, mwaka huu kuelekea nchini humo.

"Timu itaingia kambini kesho(leo) kujiandaa na mashindano ya Cosafa, ninaamini tutakwenda kuiwakilisha vizuri Tanzania kupitia mashindano hayo," alisema Pawasa.

Pawasa, pia aliwaomba wadau mbalimbali kuiunga mkono timu hiyo ili iweze kwenda kutimiza malengo yake.

Alisema michuano hiyo inatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa, jambo ambalo amewataka wachezaji kuhakikisha wanakwenda kushindana na si kushiriki.

# Straika mpya

INATOKA UK. 24

zaidi kwani inaheshimika hata na timu za Kiarabu hivi sasa," alisema.

Mbali na straika huyo, Yanga inahusishwa pia na mastraika Makabi Lilepo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, kutoka Klabu ya Al Hilal Omdurman ya Sudan na WIlliam Karamako, Muivory Coast, akiicheza Asec Mimosas.

Mchezaji huyo ameshawahi kuzichezea Klabu za Vital'O ya Burundi mwaka 2019, kabla ya kujiunga na AS Kigali ya Rwanda 2020 hadi 2021 ambapo aliendaa kucheza soka la kulipwa nchini Jordan katika Klabu ya Al Faisaly Amman 2021 hadi 2022, kabla ya kuondoka kwenda kukipiga na Klabu ya Muktijoddha Sangsad KC ya nchini Bangladesh.

Pia, mwaka huo huo wa 2022, akatoka na kujiunga na Al Naft Sport Club ya Iraq, kabla ya kujiunga na Kuching City FC ya Malaysia kwa msimu uliomalizika.

Afisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, amesema wao tayari wameshamaliza usajili kilichobaki ni kuwatangaza tu.

"Kama hao mnaowasema wamo au hawamo, lakini sisi usajili tumeshafunga, bado kuwatangaza tu, kama ni hao au wengine, lakini tutawatangaza na tutaacha baadhi ya wachezaji na wengine tutawapeleka kwa mkopo," alisema Kamwe.

# Ugumu jezi

INATOKA UK. 24

Semindu alisema alienda kupanda kwa mara ya kwanza na kufanikiwa kufika kileleni na alikuwa na bendera ya Simba ikiwa ni timu ya kwanza kupepea kwenye kilele cha mlima huo.

"Simba itakuwa timu ya kwanza kuzindua jezi katika kilele cha mlima Kilimanjaro, lakini tayari ni wa kwanza tena kwa bendera yake kupepea kwenye kilele cha mlima huo. Baada ya hapo nilirudi kupandisha tena mwaka 2020, kisha 2021 na mwaka jana pia, ndipo nikapandisha jezi za Yanga," alisema Semindu.

Alisema hadi sasa amepanda kwa zaidi ya mara 100, na kwamba ugumu wake ni kutembea umbali mrefu na mabadiliko ya hali ya hewa kwa baridi kali kuongezeka kadri wanavyosonga na kwamba kufika kileleni unatakiwa kuwa na mazoezi ya pumzi.

Aliongeza kuwa, kila mmoja anaweza kupandisha mlima huo kama akiweka nia na kufanya mazoezi ya pumzi na stamina za miguu angalau siku 60 kabla ya kuanza kupanda mlima huo.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema watu hao wanaondoka Moshi mjini saa 1:00 asubuhi ambapo watakutana na watu kutoka Hifadhi ya Taifa Tanzania (TANAPA), ambao watapandisha nao.

"Tumeamua kwenda kuzindua katika kilele cha Mlima Kilimanjaro kwa sababu ndio sehemu ya juu Afrika, ambapo kila mmoja ataona, baada ya kuzindua jezi hizi maduka yote Tanzania nzima unaweza kuipata," alisema Ahmed.

Michezo

Jumatano Julai 19, 2023
Nipashe



## Chilunda kuibukia Simba

UKURASA 23




Viongozi wa Simba wakiwa tayari wamewasili mjini Moshi jana na kibegi cha jezi, kwa ajili ya safari ya kupanda Kilele cha Mlima Kilimanjaro itakayoanza leo kwenda kuzindua jezi hizo za msimu mpya wa 2023/24. Jezi hizo zitazinduliwa katika kilele cha mlima huo Ijumaa saa 1:00 usiku na kuanza kuuzwa Jumamosi kote nchini. **MPIGAPICHA WETU**

# Ugumu jezi Simba SC kileleni Kilimanjaro

**Na Saada Akida, Moshi**

WAKATI Klabu ya Simba ikilenga kuonyesha utofauti katika uzinduzi wao wa jezi za msimu wa 2023/24, uongozi wa klabu hiyo, umeteua watu maalum kwa ajili ya kuupanda Mlima wa Kilimanjaro kwenda kuzitambulisha rasmi jezi zote tatu za msimu mpya, lakini wakieleza ugumu uliopo hadi kufika kilele cha mlima huo mrefu zaidi barani Afrika.

Safari hiyo ya kupanda mlima huo inaanza leo, wakianza Gate la Marangu kupitia Mandala na kisha watatembea kwa siku tatu hadi kufika kileleni na kuzindua jezi hizo keshokutwa Ijumaa saa 1:00 usiku.

Mmoja wa watu waliondaliwa kwa kazi hiyo maalum ni Jacob Semindu, shabiki wa Simba ambaye mwaka 2019 alikwenda kuipandisha bendera ya klabu hiyo na kuwa timu ya kwanza kuipeperusha katika mlima huo mrefu zaidi barani Afrika.

INAENDELEA UK. 23

# STRAIKA MPYA WA YANGA AFUNGUKA

●●●Hii ni klabu kubwa ambayo ukicheza unajitafutia soko la kusajiliwa na zingine kubwa zaidi, hivyo...

**Na Adam Fungamwango**

MMOJA wa mastraika anayetajwa kuwa kwenye mazungumzo na Klabu ya Yanga, kwenda kuziba nafasi ya Fiston Mayele, anayesemekana tayari amemalizana na Klabu ya Pyramids ya Misri, Sudi Abdallah, amezungumza kwa mara ya kwanza akisema anaisubiri nafasi hiyo kwa hamu kubwa.

Sudi, raia wa Burundi alisema ingawa mpaka sasa hakuna kitu kilichokamilika, lakini akipata nafasi ya kuichezea Yanga hatojiuliza mara mbili kwa sababu ni moja kati ya klabu kubwa si kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki bali kwa sasa ni Afrika nzima.

Akizungumza jana kutoka nchini Burundi, mchezaji huyo alisema kwa sasa timu hiyo ni kama njia au jukwaa kwani wachezaji wengi wa ukanda huu wanaihitaji kwa ajili ya kujitangaza.

"Hakuna kitu ambacho kimemalizika mpaka sasa, siwezi kusema kama tulionge nini na viongozi wa klabu hiyo ila tunangoja tuangalie nini kitafuata, Yanga ni timu kubwa na kila mchezaji ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati anataka kuichezea, ni klabu ambayo ukicheza unajitafutia soko la kusajili na klabu zingine kubwa zaidi, ni timu yenye mashabiki wengi na mchezaji kama ukienda kufanya vizuri unajitengenezea nafasi kubwa

UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042